# Nipashe


Jumatatu Aprili 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580919

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

CHEZA USHINDE SASA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Askofu** Shoo afunguka kuhusu mgogoro KKKT Dayosisi Konde

UKURASA 3

## IBADA ZA PASAKA

# MAASKOFU WANENA

• **Wakemea** ubadhirifu serikalini, vibanda umiza, wataka maombi kwa Ukraine... *Endelea ukurasa 2*



"Tunafundishwa ukizidiwa na jambo lolote mtegemee Mungu

**Abedinego Keshomshahara**



"Niwaombe Wakristo na Watanzania wote mwaka ni wa sensa, hivyo ni vyema wote tukajitokeza kushiriki kuhesabiwa, ili serikali iweze kupanga mipango yake ya maendeleo.

**Askofu Mteule Moravian, Lawi Mwankuga**



"Wakishatazama picha wanapata mahangaiko na kwenda kutafuta wadada poa ili watulize mihemko, ukishaumizwa na vibanda umiza unaenda kupoza na hapo yanatokea magonjwa ya zinaa.

**Askofu Mkuu Isaack Amani**



"Pamoja na jitihada za Rais Samia, bado watendaji wake wameshindwa kuwatumikia wananchi ipasavyo, tumeona matukio ya ufisadi, rushwa, uzembe kazini

**Dk. Dickson Chilongani**



"Familia nyingi zimekuwa na majaribu mengi ambayo yanasababisha watoto kutoelewana na baba, mama pamoja na wao kwa wao

**Methodius Kilain**

## Vifo vya wanyamapori barabarani vyashtua

UKURASA 7



## CAG Kichere akosoa kukosekana kanuni ulipaji wa fao WCF

UK.4


**MICHEZO** **NABI AIACHA SIMBA, AKILI KWA NAMUNGO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Maaskofu wanena ibada za Pasaka

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU na viongozi wengine wa dini wametoa ujumbe mbalimbali katika ibada za Pasaka ikiwa ni kumbukumbu ya kufufuka kwa Yesu Kristo.

Wamekemea watumishi wa umma wanaoiba fedha za umma na kuwataka kutubu haraka kabla ya adhabu, kutaka kuzuiwa vibandaumiza vinavyoonyesha picha chafu kwa watoto na vijana na kuwa na upendo huku wakiombea nchi ya Ukraine iliyovamiwa na Russia.

VIBANDA UMIZA

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaack Amani, alikemea vibandaumiza vinavyoonyesha picha za video za mitandao ya ngono kwa watoto na vijana ili kunusuru maadili yanayomomonyoka siku hadi siku.

Akihubiri kwenye mkesha wa adhimisho la misa la Sikukuu ya Pasaka lililofanyika katika Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha la Mtakatifu Teresia wa Mtoto Yesu, alisema kumekuwepo na wimbi la watoto na vijana ambao wamekuwa wakipewa pesa na wazazi na kwenda kwenye vibanda hivyo na kuangalia picha za ngono na kuwaamshia mihemko inayosababisha uhitaji wa tendo la ngono.

"Wakishatazama picha wanapata mahangaiko na kwenda kutafuta wadada poa ili watulize mihemko, ukishaumizwa na vibandaumiza unaenda kupoza na hapo yanatokea magonjwa ya zinaa,"alisema Askofu Mkuu Amani.

Aliuliza swali la kuwa viongozi wapo wapi wasizuie vibanda umiza? wazazi wapo wapi wasizuie watoto na vijana kunusuru maisha yao na kuongeza kuwa wamiliki wa vibanda hivyo hamu yao ni pesa bila kutafakari madhara ya makundi hayo na Taifa.

FEDHA ZA UMMA ZINAIBWA

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, alidai kuwa pesa nyingi za maendeleo ya nchi, zinapitishwa kwenye njia za panya na zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi.

Akitoa salam zake jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini na Dayosisi ya Kaskazini, Askofu Dk. Shoo, aliwataka wanaofanya hayo ya kujilimbikizia mali kuangalia ustawi wa nchi kwanza.

"Hayo mabilioni na matrilioni unayokusanya yatakufanyia nini? tuangalie ustawi wa nchi yetu, the common goods (mahitaji muhimu) na hili na lile ambalo limetajwa hapa ni kiburi.

"Tuache majivuno, usijione bora kuliko mwenzako hata kama una cheo gani, hata kama una nafasi gani au kama una uwezo gani. Acha majivuno, acha kujiinua, acha kiburi ni hivyo tu.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akishiriki ibada ya Misa Takatifu ya Sikukuu ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Maria Theresa Ledochowska iliyopo kiwanja cha ndege, mkoani Dodoma jana. Ibada hiyo imeongozwa na Padri Gilbert Magidale. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

"Nimesukumwa tu mambo mawili, neno moja ni ujumbe wangu ambao ni kwa Watanzania wote, haijalishi wewe ni mkristo, haijalishi wewe sio mkristo lakini kama Watanzania na neno hili ni kutoka Wafilipi 2:3-6, anasema maneno haya; Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu."

Alimtaka kila mtu amhesabu mwenzie kuwa ni bora kuliko nafsi yake na kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.

UBINAFSI UNATUTAFUNA

Aidha, Askofu Dk. Shoo, alisema ubinafsi unalitafuna taifa kutokana na watu kujilimbikizia mali na kutafuta mali za dhuluma.

Mkuu huyo wa Kanisa alisema, "Ubinafsi unatumaliza na ubinafsi ni mtego mkubwa wa shetani, unadanganywa, huamini kwamba uzima wako, furaha yako, amani yako iko ulikojilimbikizia. Kumbe haya mavitu unayojilimbikizia pasipo haki, kwa dhuluma, kwa ufisadi yatakuja kukuangamiza, yatakuja kukuondolea amani na furaha, hutayafaidi ni mtego.

"Na hili siyo tu kwa viongozi wenye mamlaka katika jamii kwa maana ya viongozi wa kisiasa, viongozi wa biashara na kampuni, hata kwa watumishi wa Mungu. Tuangalie ustawi wa kondoo wa Mungu tuliokabidhiwa, ustawi wa watu wa Mungu tuliokabidhiwa badala yetu sisi binafsi, maslahi yetu ya binafsi."

Kuhusu viongozi kujikweza, Dk. Shoo amehoji ulipowekwa kando unyenyekevu kwa viongozi.

"Unyenyekevu umeenda wapi, unyenyekevu kwa watumishi wa Mungu umeenda wapi? Mbona badala ya kuwatumikia watu wa Mungu na kusimamia yale ya kweli na haki kwa kundi la Mungu tulilokabidhiwa tunajifanya mabwana juu ya kundi la Mungu. Tunatafuta tu maslahi ya binafsi,

"Mbona watumishi wa Mungu tumefika mahali ambapo hata tunapokosea hatutaki tuambiwe Baba Askofu, Mchungaji. Kwa hiyo hapo utumishi haujaenda sawa sawa."

MAISHA YA UPENDO, VITA UKRAINE

Kanda ya Ziwa, waumini wameaswa kuishi maisha ya upendo, matumaini na kuwasha mishumaa, ili kuondoa giza katika mioyo yao huku wakitakiwa kuiombea nchi ya Ukraine ambayo imevamiwa na Russia.

Akihubiri katika misa ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mabatini jijini Mwanza, Paroko John Ebo alisema katika kipindi cha Pasaka waumini wanatakiwa kuvaa upendo na matumaini mapya.

Alisema vitu hivyo ni muhimu kwa kuwa vinabeba maisha ya kila siku ya mwanadamu na katika kipindi hiki vinakumbusha watu kwamba Yesu Kristo alifufuka katika mioyo yao.

Akizungumzia suala la vita vya Ukraine na Russia, Paroko huyo alisema, watu wote duniani wanatakiwa kuwaombea wananchi wa mataifa hayo na kwamba ni mbaya kwa kuwa imepiganwa kipindi cha Kwaresma.

Paroko Msaidizi wa Parokia ya Nyakahoja Jimbo Kuu la Mwanza, leo Amani alisema vita ya Ukraine inatoa funzo muhimu katika maisha ya duniani kwa kuwa wanaoangamia ni wanadamu wenzetu, na kutaka kuwaombea ili Mungu awasamehe walioanzisha vita hiyo.

Akizungumzia suala la upendo, Paroko Amani alisema, suala hilo likifanywa na binadamu halina hasara yoyote kwa mtu, huku akitaka kuwashwa mishumaa ili kuondoa giza na kuleta upendo na furaha kwa watu.

MAISHA YA KUMPENDEZA MUNGU

Askofu Liberatus Sangu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga mkoani Shinyanga, akitoa mahubiri katika Misa ya Pasaka kwenye mkesha wa Kanisa la Mama Mwenye Huruma Parokia ya Ngokolo mjini Shinyanga, aliwaasa Watanzania kuishi maisha yaliyo ndani ya Kristo kupitia Roho Mtakatifu.

Aliwataka wafanye hivyo ili waweze kuishi katika furaha, upendo, upole, uvumilivu, utu, wema, uaminifu na kudumisha amani.

Alisema kuishi maisha ya Kristo ni kuongozwa na roho mtakatifu na kutenda mema na kwamba kwa kufanya hivyo kutaondoa mifarakano, chuki, fitina, uchochezi, wivu, hasira, ugomvi, ulevi na ushirikina.

Katika hatua nyingine aliwataka Watanzania waishi kwa kupendana pamoja na kusaidia watu wenye uhitaji, kama alivyokuwa akifanya Kristo ili kupata fadhila zake na maisha yao kuwa ya mbaraka.

Akitoa mahubiri kwa waumini katika Kanisa la Katoliki la Bunena Parokia ya Bukoba, Askofu Askofu Msaidizi wa Jimbo la Bukoba mkoani Kagera, Methodius Kilaini, alisema vinapotokea vikwazo katika imani ni vyema kumuomba Yesu na mama yake Maria aweze kusaidia.

Aliwataka waumini kuishi kwa upendo, kuamini na kumcha Mungu kuanzia katika familia zao ili kuleta furaha kama jinsi Yesu alivyojitoa kwa ajili ya ukombozi wa dhambi za wanadamu.

Alitoa kauli hiyo, katika misa ya Pasaka na kusema kuwa familia nyingi zimekuwa na majaribu mengi ambayo yanasababisha watoto kutoelewana na baba, mama pamoja na wao kwa wao.

Kwa upande wake, Askofu wa Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Abedinego Keshomshahara, alisema wanadamu wanapaswa kuishi kama alivyoishi Yesu Kristo hapa duniani.

RUWA'ICHI ATAKA MATENDO MEMA

Naye, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddaeus Ruwa'ichi, aliwasihi waumini wa Kikrito kuendelea kuwa mashahidi wa Yesu kwa kutenda mambo mema na kuacha kutenda dhambi kwa kuwa kufanya hivyo ni kumkana Yesu Kristo.

"Je ni mara ngapi nimemkana Yesu, katika mambo makubwa na madogo,ni mara ngapi nimemkana kwamba simjui, simfahamu, sifuatani naye"

Aliongeza kuwa katika kuadhimisha fumbo la pasaka kila mmoja anatumwa shahidi wa fumbo hilo kwa kulitangaza kwa walimwengu, kwa kuhubiri habari njema ambayo ni Kristo aliteswa, Kristo alikufa, Kristo amefufuka, ni mshindi, ni Mtukufu.

KUMUOMBEA RAIS

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Ruvuma, Amon Mwenda, aliwataka Watanzania kuona umuhimu wa kumuomba Mungu ili aendelee kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuongoza nchi ya Tanzania kwa kudumisha amani iliyopo na kuwakataa watu wenye nia mbaya ya kuivuruga amani ambayo tulipewa na Mwenyezi Mungu.

**■Imeandikwa na Richard Makore (MWANZA), Godfrey Mushi (MOSHI), Daniel Sabuni, (ARUSHA), Marco Maduhu (SHINYANGA) , Restuta Damiani (BUKOBA) Jenifer Gilla (DAR) na Gideon Mwakanosya (SONGEA).**

HABARI KITAIFA

# Askofu Shoo afunguka mgogoro wa KKKT

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema baada ya mgogoro wa kiutawala kuitikisa Dayosisi ya Konde, wiki mbili zilizopita, amani imerejea kwa asilimia 98 katika sharika zinazounda dayosisi hiyo iliyopo mkoani Mbeya.

Pia, alitangaza wakati wowote Askofu mpya Mteule Mch. Geofrey Mwakihaba, atawekwa wakfu kuiongoza dayosisi hiyo pamoja na kuingiza viongozi wengine wapya kazini.

Askofu Dk. Shoo, alifunguka kwa mara ya kwanza kuhusu mgogoro huo jana, wakati akitoa salaam za Sikukuu ya Pasaka ya Kufufuka Yesu Kristo, ibada iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini wa Dayosisi ya Kaskazini.

Askofu Mteule Mwakihaba, alichaguliwa Machi 24, mwaka huu, baada ya kung'olewa madarakani aliyekuwa Askofu wa Dayosisi hiyo, Edward Mwaikali.

"Sisi tumesema tunasonga mbele, wana-Konde amani imerejea, yaani katika sharika asilimia 98 imerejea, wanasema tunatambua uongozi kwa sababu ni sisi tuliochagua viongozi wapya. Ndugu zangu wapendwa, tunasema tutasonga mbele na tumeshaweka tarehe dayosisi ile imeshapanga, viongozi wapya watabarikiwa tu.

"Tutamuweka wakfu askofu mpya na kuingiza viongozi wapya kazini. Nawaomba endeleeni kuwaombea wale wenzetu, endeleeni kutuombea viongozi wa kanisa, lakini pia endeleeni kuomba kwa ajili ya roho hii ambayo imejiinua kwa sababu wanazozijua wao kwa kutaka tu kwa makusudi kuchafua kanisa."

Akichambua mgogoro huo ulivyokuwa, Askofu Dk. Shoo, alisema unaumiza kundi la Bwana na kanisa.

"Ninajua kwa KKKT, mmeona kwa majuma mawili hivi, kuna mambo yameandikwa kwenye magazeti. Watu wengi wameniuliza nini kinachoendelea; mimi naona kiini chake ni hapo hapo, watumishi wa Mungu ambao tumesahau wajibu wetu na nafasi yetu. Tunalikosea kundi la Bwana hivi hivi, tunakanyaga katiba za dayosisi zetu hivi hivi, halafu tunapoambiwa tunakosea tunavunja heshima, tunapeleka kanisa mahakamani, tunatoa habari za uongo na za kupotosha.

"Nafikiri ninyi mlio makini kama mmesoma hasa zinazoandikwa na gazeti moja, yapo magazeti mawili yanaandika hayo mambo. Muelewe kwamba hawa ni wachache, wachache tu ambao wameamua kutumia mahakama, wameamua kutumia magazeti kulichafua kanisa la Bwana.

"Lakini nipende tu kuwaambia kule kwenye Dayosisi ya Konde, yale yanayoelezwa kwenye magazeti sivyo yalivyo. Mnayoelezwa kwenye magazeti ni uongo, ni propaganda, kikundi kidogo kimeamua vita ya magazeti, sisi tumesema waendelee tu, lakini wale tunaofahamu ukweli, tunaofahamu haki, nini kilichotendeka, sisi tuna amani.

"Kwa hiyo ningewaomba sana kwanza muyapuuzie hayo ambayo yanaandikwa, ukisoma kwa makini utajua tu kwamba ni habari za upande mmoja za vikundi vichache, bahati mbaya sana kuna maaskofu wawili, watatu.

Kwa hiyo kikundi kidogo cha wanaopigania nafasi zao, badala ya kujishusha na kutubu kwamba hapa tumekosea wanazidi kujiinua, lakini bila kusahau marafiki zao wachache ambao wanasema eti tunalindana. Maaskofu tunalindana, tunalindana katika uongo, tulindane katika kulitesa kanisa la Mungu? Mimi nasema hapana!

"Na maaskofu wengi wa KKKT na wale washarika wa kule Konde wamesema hapana. Sababu nyingine nahisi hao hao wanaopeleka habari za kwenye magazeti ni kutaka tu kulichafua kanisa."

**KANISA LINAPITA MAPITO**

Vilevile, Askofu Dk. Shoo alisema; "Mimi nimesema tushindane na mambo mengine, tusishindane na mambo ya Bwana, Yesu alijua atasulubiwa, tunafahamu kanisa litapita katika mapito, lakini Yesu akasema ole wake yeye amsalitiye mwana wa Adamu na mimi nasema ole wake yeye ambaye kwa makusudi kabisa anataka kulichafua Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

"Ndugu zangu wapendwa, kilichofanyika kule Dayossi ya Konde, kimefuata taratibu zote, tumekwenda hatua kwa hatua tena kwa maombi, mkutano mkuu ukakaa, mkutano wa kihalali kabisa, mkutano ambao askofu ambaye ameamaliza muda wake, ambaye hakuchaguliwa alisaini makubaliano kwamba mkutano huu tuufanye mkutano mkuu.

"Tuunde kamati ya mkutano mkuu, akasaini yeye mwenyewe ikaundwa kamati. Kamati hii iandae mkutano mkuu ambao unaleta wana Konde wote pamoja ili waamue wao wenyewe, kwa sababu jambo la wana Konde linamalizwa na wana Konde wenyewe na sisi hicho ndicho tulichokiheshimu.

Askofu baadaye akamua kuleta majina ya wajumbe wa kamati siku moja kabla kamati haijamaliza kazi yake. Ameacha kuleta wale wajumbe ameenda mahakamani kuzuia mkutano usifanyike.

"Mungu ashukuriwe, mahakama imesikiliza ikatupilia mbali, madai na mashtaka yale kwamba eti mkutano mkuu usifanyike. Mimi nikajiuliza, sasa mkutano mkuu ule ndiyo wa kuwaleta pande zote mbili zinazolumbana?

"Ndiyo pekee unaoweza kuwaleta pamoja wakaamue kuhusu hatima ya Dayosisi yao. Waamue kiti kibaki kule kilikopelekwa ama kirudi kule kilikokuwa. Mkutano mkuu ndiyo wenye uamuzi. Askofu anakacha mkutano mkuu anataka kuzuia usifanyike na halmashauri kuu yake nao wanaungana naye ni kwa sababu walijua walikosea tangu mwanzo.

Jambo la kuhamishwa makao makuu ya Dayosisi ya Konde kutoka Tukuyu Mbeya, lilishazungumzwa kwenye mikutano mikuu mitatu. Na mikutano yote mikuu mitatu ya Dayosisi ikikataa. Badala ya kukaa na kuwasikiliza Wachungaji maoni yao, wanawafukuza uchungaji, wanawatenga. Sasa hiyo ndiyo namna ya kwenda kama Kanisa? Kwa hiyo mgogoro wenyewe chanzo chake ni hapo."

**MADARAKA YAMEWALEVYA**

Kuhusu kiini cha mgogoro, Askofu Dk. Shoo alisema: "Tumetumia vibaya madaraka yetu, hatukutumia vyombo vile vya kikanisa vinavyotakiwa, basi mkutano mkuu uliokaa ni mkutano halali. Kwa sababu wao ndiyo waliokwenda mahakamani wakaambiwa hapana, mkutano huu ni halali, hakimu akasema haoni sababu kwa nini mkutano huu usifanyike.

"Wakakaa wana Konde wenyewe, sisi tulikuwa waangalizi tu wakasema kama ni mwenyekiti ambaye ni Askofu hajaja, sisi tunachagua mwenyekiti wetu, wakachagua mwenyekiti mkutano ukaendelea na ndipo mkutano ukafikia maamuzi yaliyofikiwa.

"Mimi nasema wana Konde wamekwishakuamua, wamechagua askofu mpya, wamechagua msaidizi wa askofu mpya, halmashauri kuu mpya kwa mkutano mkuu halali uliokuwa na akidi.

"Sasa sisi tumeambiwa tumepelekwa tena mahakamani na mtu mmoja tu Askofu aliyemaliza muda wake na kimsingi mkutano mkuu wa Dayosisi ulikuwa ufanyike mwaka jana, kwa sababu kipindi cha uongozi kilikuwa kimeisha. Sasa hatujui kama wamefanya hivyo kwa ajili ya kuvuta kipindi cha uongozi. Kwa hiyo hata ile Halmashauri Kuu kwa mujibu wa katiba yao



Askofu Dk. Frederick Shoo,


**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD**

CRB TANZANIA

**REGISTRATION STATUS UPDATE**

The Board would like to inform all contractors registered in **CLASS FIVE** as of 30.06.2017 that Pursuant to section 4(q) of the Contractor Registration Act No. 17 of 1997, it is now updating contractors' information in the database to match with the current status of the contractor in terms of shareholding status, official addresses, staffing level and equipment holding capacity.

In order for the said information to be effectively and timely updated, the said contractors are hereby instructed to submit the duly filled **REVIEW INFORMATION FORM (already posted in your postal addresses and can also be downloaded on the website www.crb.go.tz**).

In addition, the following information should be submitted along with the said form:

1. Current Business Registration and Licensing Authority (BRELA) Search Report.
2. Covering letter indicating inter alia, which names among the shareholders shown in the Brela search, stands as Managing and Technical Director in the construction company.
3. Resolution of the Board of Directors and Affidavit as a commitment that the submitted information is correct and can be used to update your company status in the data base.

The said information should reach the Board latest by 30th April 2022.

**REGISTRAR**

216795702



Naibu Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof. Patrick Nsimama (wa pili kushoto) akitoa cheti kwa mwanafunzi, Midina Yattani wa Chuo cha Meru National Polytechnic Kenya, baada ya mafunzo ya siku 10 kutoka kituo cha umahiri wa mambo ya TEHAMA (ITCOEICT), jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CAG akosa kanuni ulipaji wa fao WCF

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kutokuwapo kwa kanuni kwenye Fao la Utengemao katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne iliyopita, CAG Charles Kichere anasema fao hilo linahusisha shughuli zozote zinazojaribu kurejesha watu wanaopata ulemavu wakiwa kazini kwenye utimamu wao wa kimwili, kiakili na kijamii.

Anasema Kanuni ya 31(4) ya Kanuni za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi za mwaka 2016 inabainisha kuwa malipo ya Fao la Utengemao yataanza wakati ambapo waziri mwenye dhamana ametoa kanuni maalumu kwa ajili ya fao hilo baada ya kushauriwa na bodi.

"Mfuko ulikuwa na matukio ya wafanyakazi 92 waliopata ulemavu wakiwa kazini na waliohitaji kufidiwa. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2021, WCF ilikuwa haujaanza kulipa mafao ya utengemao kwa jamii na shughuli zingine zinazohusiana kwa sababu ya kukosekana kwa kanuni za fao hili.

"Kutokuwapo kwa kanuni zinazosimamia Fao la Utengemao kwa jamii linazuia ulipaji wa mafao hayo kwa walengwa. Ninapendekeza WCF wamshauri waziri mwenye dhamana aandae na aidhinishe kanuni za fao hilo.

**WAAJIRI KUTOKUJULIKANA**

CAG pia anasema Kifungu cha 71(1) cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2015 kinaeleza kuwa, mwajiri anayefanya biashara Tanzania, atalazimika kujisajili kwa Mkurugenzi mkuu wa WCF ndani ya muda uliowekwa na katika fomu iliyowekwa.

"Mapitio yangu ya uendeshaji wa WCF yalibaini kuwa, hadi tarehe 30 Juni 2021, mfuko ulikuwa na waajiri 6,240 ambao hawakulipa ada ya michango ipatayo Sh. bilioni 6.37 kwa muda wa kipindi cha kuanzia miaka miwili hadi mitano.

"Mathalani, Bodi ya Ustawi wa Jamii ya Aga Khan Tanzania (kampuni binafsi) ilikuwa haijalipa ada ya michango tangu tarehe 28 Mei 2016 na Kampuni ya UTT (kampuni ya umma) ilikuwa haijalipa ada ya michango tangu tarehe 28 Juni 2018.

"Nilibaini pia kuwa, WCF haukuwa umetambua mwenendo wa utendaji kazi (kama ofisi bado zinafanya kazi au kufungwa) na waajiri hao.

"Nina shaka kuwa kutokujua kama mwajiri asiyelipa ada za michango kwa muda mrefu bado anaendelea na shughuli zake ama la kunapotosha taarifa za mfuko za wanachama walio hai.

"Pia, hali hii inaathiri uamuzi wa mfuko na serikali kuhusu usajili wa waajiri wa WCF. Ninapendekeza mfuko kushirikiana na mamlaka zingine, ubaini kama waajiri ambao hawajalipa ada za michango kwa muda mrefu bado ofisi zao zinafanya kazi au zimefungwa na uchukue hatua zinazofaa," CAG anatoa hoja.

## Mbaroni madai yakukutwa na meno, nyama kilo 90

**Na Neema Hussein,** KATAVI

Jeshi la Polisi mkoa wa Katavi linamshikilia Mashaka Mavunue (42), mkazi wa Mtakuja Halmashauri ya Nsimbo kwa kudaiwa kukutwa na meno mawili yadhaniwayo kuwa ya tembo yenye uzito wa kilogramu 3.1 na nyama ya tembo kilo 90.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema jana kuwa pia mtuhumiwa alikutwa na silaha aina ya gobore, panga moja na kisu kimoja.

Kamanda Makame alisema mtuhumiwa alikamatwa Aprili 13,2022 maeneo ya Kashoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Alisema mtuhumiwa aliingia ndani ya hifadhi akiwa na silaha hizo na alifanikiwa kumpiga na kumuua mnyama huyo kisha kutoa meno yake na kubeba nyama yake kilo hizo 90.

Mbali na tukio hilo pia Kamanda Makame ametoa taarifa ya hali ya usalama barabarani ambapo amesema wamefanikiwa kukamata vyombo 501 vya usafiri vikiwa na makosa mbalimbali ya usalama barabarani.

Alisema ndani ya vyombo hivyo 501 magari ni 236 na pikipiki ni 265.

Aidha alisema katika kuhakikisha wanakabiliana na changamoto za usalama barabarani, wanaendelea kutoa elimu kwa madereva na kuvikagua vyombo hivyo mara kwa mara.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe**

**Kituo cha njombe mjini**
**Mkoa wa njombe**

**Usimamizi wa mirathi na 21/2022**

**Romward Francis Kinyero……marehemu**

**Tobiath Japhari Mohamed…………msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 14th ya mwezi wa mei mwaka 2022

Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 14th aprili mwaka 2022.

Hakimu Mkazi
HAKIMU MKAZI
NJOMBE - MJINI



**KUPOTEA KWA CHETI**



Ndugu, **BONIPHACE KABELELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye **index no S.4811/0106** Kilichotolewa na baraza la mitihani NECTA, chenye **no CS16000112904** katika shule ya Bidii sekondari Mkoa wa Mwanza Mwaka 2016. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Control No 9910817967960.**



**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI BAJAJ BOXER**

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki bajaj boxer yenye usajili namba **T350 CTV, CHASSIS NAMBA: MD2A21BZ3DWH78082, ENGINE NAMBA : PFZWDH42418.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/148530/2022**



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 42 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**FERICK ASANGALWISYE KYAMBA**

- **DORIS ADAMSON MWANJELA**
- ……………………………………………

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant (of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **20th Day of April 2022**

Dated at Morogoro this April day of 1st day of 2022.

RESIDENT MAGISTRATE



KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD
COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 16/05/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA MERCEDES BENZ 200. T 333 DSB, MALI YA CONRAD LUCAS LIKOTIKO BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, P.O. BOX4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**



**TAARIFA YA KUFUNGA KAMPUNI**

Wamiliki wa Kampuni ya Starise Edutainment (T) Limited yenye Namba za usajili 139184432 ya Mei 18, 2019, Wanapenda kuutangazia Umma kuwa kampuni yao haikuweza kufanikiwa kuanzisha Biashara kama ilivyokuwa matarajio yao, hivyo kuamua kuifunga kampuni kwa hiari.

**C/O JOHN BISEKO**
**S.L.P 395**
**DODOMA**



Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Iringa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mohamed Moyo (mwenye kapelo) akikagua miradi ya afya jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Abiria wapinga mapendekezo ya nauli

**Na Jenifer Gilla**

WIKI iliyopita katika mkutano na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), wamiliki wa vyombo vya usafiri nchini, waliomba kupandishwa bei za usafiri huo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha ikilinganishwa na miaka 10 iliyopita wakati nauli ilivyopangwa.

Akiongea na Nipashe wakati wa mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi nchini (TABOA), Abdalah Kiongozi, alisema kuwa wameshauri nauli iongezeke kuanzia asilimia 34 hadi 54 kulingana na kila kilometa, akitoa mfano nauli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa sasa ni Sh. 60,000, na kupendekeza iongezeke hadi Sh. 80,000.

Kwa upande wa daladala kwa jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA), Sabri Mabruk, alisema wamependekeza ongezeko la nauli umbali wa kilometa 10 iwe Sh. 745.00, kilometa 15, Sh. 1,117.40. Kilometa 20, Sh. 1,490, kilometa 25, Sh. 1,862.50 na kilomita 30 iwe Sh. 2,235 huku wanafunzi walipie nusu ya gharama hizo.

Tangu mapendekezo hayo yatolewe kumekuwa na manung'uniko kutoka kwa watumiaji wa vyombo hivyo ambao baadhi yao walizungumza na gazeti hili na baadhi yao akiwamo Husein Shabani, mkazi wa Tabata Kinyerezi alisema, ongezeko hilo ni kubwa hasa kwa kipindi hiki ambacho kuna mfumuko wa bei ya bidhaa muhimu katika familia na kuiomba serikali kufikiria wananchi wake kabla ya kuamua kuipitisha.

"Nilivyoona haya mapendekezo ya nauli za daladala kwa kweli mwili ulikufa ganzi nikajifikiria mimi ninayeishi Kinyerezi na kufanya kazi Posta, nitalazimika kugharamia siyo chini ya Sh. 2,000 kila siku kwa nauli pekee, huku vyakula navyo vimepanda, ukizingatia kuwa wakati hivyo vyote vinapanda mishahara haipandi, tunaomba serikali ituangalie wakati inafanya uamuzi katika hili," alisema Husein.

Naye Amina Enea, mkazi wa Boko (33), alisema anafahamu kuwa nauli lazima ipande kwa kuwa gharama za mafuta pamoja na shughuli za uendeshaji wa magari hayo zimepanda, lakini mapendekezo ya wamiliki wa magari ni makubwa kama yakipitishwa yatakuwa ni kuongeza uchungu kwenye kidonda.

Flora Peter (40), Mkazi wa Korogwe, Wilaya ya Tanga, alisema kuwa kupanda kwa nauli za mabasi yanayokwenda mikoani kutaathiri biashara zake kwa kuwa mara nyingi husafiri kwenda jijini Dar es Salaam kukusanya biashara na kuuza kijijini kwake.

"Kwa mimi ambaye kwa wiki nakuja Dar es Salaam kukusanya mizigo mara tatu naona kuwa nitaathirika kwa kuwa sitoweza kulipa zaidi ya Sh. 15,000 ninayolipa sasa, itanilazimu kupunguza safari zangu za kuja huko au kuongeza bei za bidhaa ninazouza ili kufidia nauli, wacha tuone hali itakuwaje," alisema Flora.

Janeth Mwaimu (16), mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Zawadi alisema kuwa kupandishwa kwa nauli ya wanafunzi kutakuwa ni mzigo kwa wazazi hasa wale wanaosoma shule za mbali ambao hulazimika kupanda basi zaidi ya moja.

"Mimi naona wapandishe tu nauli za watu wazima na kuwaacha wanafunzi kwa sababu mzigo wote huo utamwangukia mzazi tu, kuna wanafunzi hapa tunasoma nao wanapanda basi tatu hadi kufika shule, sasa mfano kila basi akilipa Sh. 350 kwa huo umbali wa kilomita 10, kwenda na kurudi atalazimika kulipa Sh. 2,000 hapo bado hajala," alisema Janeth.

# Mgambo waliopora machinga watimuliwa

**Na Richard Makore,**
MWANZA

SAKATA la askari mgambo wa Jiji la Mwanza kupora ndizi za machinga na kuzirusha ndani ya gari na kuondoka nazo, limechukua sura mpya, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, kuagiza mgambo waliohusika kufukuzwa kazi pamoja na mratibu wa jiji.

Akizungumza jijini Mwanza na waandishi wa habari jana, Gabriel alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makiligi, kuwafukuza kazi askari hao pamoja na kumsimamisha kazi mratibu wa machinga Jiji la Mwanza.

Alisema kitendo kilichofanywa na askari hao siyo maagizo ya serikali katika kuwapanga machinga, na kwamba wamekiuka maadili ya kazi zao.

"Naagiza Mkuu wa Wilaya awavue na awaondolee hadhi ya kuwa askari wa jeshi la akiba la mgambo mara moja kuanzia leo (jana), lakini pia namsimamisha kazi mratibu wa zoezi la kupanga machinga Jiji la Mwanza kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake," alisema.

Tukio hilo ambalo lilisambaa katika mitandao ya kijamii, limemuibua Gabriel siku moja baada ya kutokea kwake

Mwishoni mwa wiki, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alimuagiza Gabriel kujitathmini kutokana na sakata la machinga kuporwa ndizi zake.

Alisema siyo maagizo ya serikali kufanyika vitendo hivyo dhidi ya machinga na kuagiza zichukuliwe hatua kali kwa waliohusika.

Bashungwa juzi aliandika katika ukurasa wake wa Instagram akilaani tukio hilo na kuagiza viongozi wa Mkoa wa Mwanza kujitathmini.

# Prof Ngowi: Mambo ya kuzingatia mpango wa biashara

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA mwendelezo wa mafunzo ya aliyekuwa Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, marehemu Prof. Honest Ngowi, leo tunaangazia moja ya masomo muhimu kwa wanaoanza biashara.

Prof. Ngowi alielezea mpango wa biashara kuwa ni andiko linaloelezea kwa undani biashara inayofanywa na mhusika. Kama mtu ana biashara kumi au ishirini kila moja inapaswa iwe na mpango wake ikielezea kwa undani mambo makuu yanayohitajika na jinsi itakavyofanyika.

"Mpango wa biashara unatakiwa uelezee biashara inajihusisha na nini? Wateja ni kina nani? Masoko ni yapi? Washindani ni wapi? Tofauti yake na biashara nyingine ni ipi?

Alisema kuwa utafiti unaonyesha kuwa wafanyabiashara wengi nchini, hasa wadogo na wakati wanaendesha shughuli zao bila kuwa na mpango wa biashara hali inayosababisha biashara zao kutokuwa na mwelekeo unaohitajika.

"Mtu amewekeza katika hoteli kubwa, amewekeza katika shamba kubwa, amewekeza katika kiwanda kikubwa, duka kubwa, lakini ukimuuliza sasa naomba mpango wa kibiashara unaoongoza maendeleo ya biashara hii, hakuna," alisema.

Mchumi huyo alieleza faida ya kuwa na mpango huo kuwa ni kumwezesha mjasiriamali kuwa na mpango makini kwa kuwa humpa mwongozo wa wapi anatakiwa kuelekea na ili afike huko anatakiwa kufanya nini sasa.

Faida nyingine kwa mujibu wa mchumi huyo ni kumsaidia mjasiriamali kupata pesa katika taasisi za fedha kwa kuwa moja ya vigezo muhimu ambavyo mjasiriamali atatakiwa awe navyo wakati anaomba mkopo ni mpango wa biashara.

"Mpango wa biashara ni muhimu kwako wewe ambaye siku moja utataka ukapate mkopo, ukapate fedha huko katika masoko ya fedha, kwa hivyo ni lazima uwe nao ili kuwaonyesha watoa fedha ni kwa namna gani utakwenda kuifanya hiyo biashara," alifafanua.

Alisema pia mpango wa fedha humrahisishia mfanyabiashara katika mchakato wa kupata wawekezaji, kwa kuwa itaonyesha anataka mwekezaji wa biashara ipi, mkubwa au mdogo, na nini matarajio ya huo uwekezaji baada ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa Prof. Ngowi kuna mambo muhimu matatu yanayohitajika kuwapo katika mpango wa biashara ili iwe na ubora unaohitajika.

Alitaja la kwanza kuwa ni kuielezea taswira ya kampuni ili watu waifahamu. Hapo mjasiriamali anapaswa kuandika kampuni hiyo inajihusisha na nini? Mitizamo yake ni nini? Mipango ya muda mrefu na mfupi.

Jambo lingine muhimu Prof. Ngowi alisema kuwa ni kuielezea biashara yenyewe, kama ni hoteli unaielezea kama ni ya utalii au ya kawaida, ni huduma gani zitatolewa ili watu waweze kuelewa kuwa ni hoteli ya nyota moja, mbili au nne.

Maelezo kuhusu soko la biashara alilitaja kuwa ni jambo lingine muhimu kuwapo katika andiko hilo. Humo itaelezwa walengwa wa biashara, kama ni shule basi ni kwa ajili ya wateja wa kimataifa au kitaifa, inafuata mitaala ya Tanzania, Kenya, Uingereza au Marekani. Haya yote yatakusaidia katika kupata wateja unaowataka.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF lindeni juhudi za Simba kwa wawakilishi bora CAF

**NI** rasmi sasa kwa mara nyingine Tanzania itawakilishwa na klabu nne kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao wa 2022/23, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Hiyo ni kutokana na juhudi kubwa zilizofanywa tena na Klabu ya Simba kwa kufanikiwa kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo kuiongezea Tanzania pointi nyingi na kuwa miongoni mwa timu 12 Afrika zitakazoingiza timu nne kila moja msimu ujao.

Huo utakuwa ni msimu wa tatu juhudi za Simba zinaipa nafasi Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya hadhi ya juu na utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Hata hivyo, licha ya juhudi hizo za Simba katika misimu hiyo miwili, huu na uliopita, ambao Tanzania iliingiza timu nne, bado wawakilishi wengine watatu, wameshindwa kuzitendea haki nafasi hizo kutokana na kutolewa mapema.

Msimu uliopita, ambao Tanzania kwa mara ya kwanza iliingiza timu nne kwenye michuano hiyo, ambazo ni 'wapiganaji' wenyewe Simba, Yanga, Azam na Namungo FC, wawakilishi hao hawakuzitendea haki nafasi hizo.

Mbali ya Simba iliyofika robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa, ni Namungo pekee ambayo ilijitutumua na kutinga hatua ya makundi kabla ya kuishia hapo, wakati ikishiriki Kombe la Shirikisho Afrika huku zingine zikiishia hatua ya wali.

Yanga ambayo nayo ilikuwa ikiiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa iliishia hatua ya awali wakati Azam FC kwenye Kombe la Shirikisho msimu huo nayo iliishia hatua hiyo ya awali.

Msimu huu tena, Simba na Yanga zikabeba jukumu la kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati Azam na Biashara United zikiiwakilisha nchi katika michuano ya Kombe la Shirikisho.

Yanga iliishia hatua ya awali wakati Simba iliyoanzia raundi ya kwanza ikashindwa kufuzu, lakini ikanufaika na kanuni za mashindano hayo, hivyo kuangukia mechi za mchujo na kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho ambapo kwa sasa ipo robo fainali.

Biashara United, ilionesha ni wapi wakongwe Yanga, na Azam FC wanakosea, baada ya kutinga kucheza mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi na mchezo wa kwanza nyumbani ikashinda mabao 2-0 dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya.

Hata hivyo, kutokana na uchanga wao uliochangiwa pia na kutokuwa vizuri kiuchumi, Biashara United ilishindwa kwenda Libya kwenye mechi ya marudiano kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kukosa kibali cha kutumia anga ya Sudan na Libya kutokana na kuchelewa kuomba kibali kwa shirika la ndege waliyokodi.


Lakini hayo yote yalitokana na hali yao kiuchumi kuwa yakulegalega, hivyo kushindwa kusafiri mapema tayari kwa mchezo huo, jambo ambalo Shirikisho la Soka Afrika (CAF), liliiondoa katika michuano hiyo na tiketi hiyo kuangukia Al Ahli Tripoli ambayo hadi sasa nayo ipo hatua ya robo fainali.

Hivyo, hizi ni nafasi ambazo Shirikisho la Soka nchini (TFF), linapaswa kuwa makini katika kupata wawakilishi wa nchi kwenye michuano hiyo, ambao wataweza kwenda kutoa ushindani na kuzilinda nafasi hizo nne.

Pamoja na utaratibu wa namna ya kuwapata wawakilishi wetu kwenye michuano hiyo ya CAF, sisi tunaona ni wakati sasa TFF ikajikita katika kufanya tathimini ya kina hasa kwa upande wa uwezo wa kiuchumi kwa kila klabu itakayokata tiketi ya kushiriki michuano hiyo, kabla ya kupeleka majina CAF.

Lakini pia tunazitaka klabu zitakazokata tiketi ya kushiriki michuano hiyo msimu ujao, kujitathimini zenyewe kiuchumi na endapo kuna itakayoona ni kina kirefu kutokana na kutomudu gharama, zitoe nafasi hiyo kwa zenye uwezo huo, huku maandalizi yakianza mapema kwa wawakilishi wetu wote ikiwa ni pamoja na kufanya usajili unaolenga zaidi michuano hiyo ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mastraika Bongo bebeni alichokifanya Mane

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ni dakika ya 18, kipa wa Manchester City, Zack Steffen alipokuwa na mpira mguuni, akiwa hana hili wala lile. Alidhani wachezaji wote 21 waliokuwa mbele yake wanamsubiri apige mpira mbele.

Macho yake hayakumuona Sadio Mane aliyekuwa anamnyemelea, na baada ya kuwa na uhakika kwamba akili ya kipa huyo ilikuwa kwa atakayempigia kuliko mpira wenyewe aliongeza kasi.

Wakati kipa akishtukia Mane yuko karibu, akahamaki na kabla ya kuwa na akili ya kutaka kumpiga chenga, aliserereka mguu wake ukifuata mpira na alipogusa, ukambabatiza mwenyewe na kutinga wavuni, likiwa ni bao la pili kwa Liverpool.

Ni bao ambalo halikutegemewa. Na wala si bao ambalo limetengenezwa au kocha amefundisha mazoezini. Pamoja na kwamba alifunga lingine, lakini hilo lilichangia Liverpool kushinda 3-2 kwenye nusu fainali Kombe la FA.

Ni utayari, kujituma na kasi ya straika, ambaye muda wote anatakiwa awe na mbinu ya kufunga mabao kwa njia yoyote ile. Nimelielezea bao hilo kwa sababu nataka kutoa somo kwa mastraika wetu Tanzania. Kwa miaka ya hivi karibuni huwezi kuliona bao kama lile, labda kwa mtu mmoja tu, Meddie Kagere.

Yeye pekee ndiye straika anayeweza kumfuata kipa kwa namna ambayo inawafanya wakati mwingine wafanye makosa.

Rejea kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba na Mbabane Swallows ya Eswatini Novemba 28, 2018, iliposhinda mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Moja ya bao lililofungwa ni kwamba, kipa wa wageni alipokea mpira hakujua kama atafuatwa na mchezaji yeyote.

Kagere alipomfuata na ghafla alipotambua hilo, akashtuka. Chochote alichotaka kukifanya hakikuwa, kwani aliteleza na kumpa nafasi straika huyo kuufikia mpira kabla ya kuujaza wavuni.

Kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, iliyochezwa Aprili 3, mwaka huu kati ya Simba na US Gendarmerie, Kagere alisababisha kipa wa timu hiyo kujichanganya na kujifunga mwenyewe kutokana na mbio alizokuwa akija nazo kumfuata.

Ukiacha straika huyo, sijawahi kuona straika yeyote Mtanzania, au mgeni anayecheza kwenye ardhi ya Tanzania mwenye uthubutu huo. Si kama hawafuati, la hasha. Wengi wanawafuata makipa kivivu au ili mradi tu na kupigwa chenga kirahisi.

Kagere humkimbiza kipa kwa kasi na nguvu. Si mara zote anafanikiwa, lakini inavyoonekana kama angeweza kupata wenzake ambao wanaweza kufanya kazi kama yeye, angekuwa anafanikiwa sana.

Kwa sasa umri umeenda, kama angekuwa straika kijana na tabia ile aliyonayo, basi angekuwa hatari mno kwa makipa. Wala isidhaniwe kuwa ni Mane tu kwa sababu anacheza Ulaya, zamani Tanzania kulikuwa na mastraika wenye tabia hizo na walifunga sana mabao ya aina ile, wakiongozwa na Victor Mkanwa, Abdallah Buruani, Adam Sabu, na wengineo. Hawa walikuwa ni hatari kwa mipira ambayo kipa anakuwa nayo miguuni, au amerudishiwa. Hawapigwi chenga kirahisi, mabao yao mengi yalikuwa ya aina hiyo.

Kwa alichokifanya Mane Ijumaa nchini Uingereza, ni funzo kwa mastraika wetu wa sasa hasa wa Kitanzania kuwa ili ujitume na kupambana.

Mastraika wa Kibongo wanataka kufunga mabao rahisi, ya kutafuniwa, na si ya kujituma kwa kupambana kama alivyofanya Mane.

Ukiangalia si wengi wanaopiga mashuti makali nje ya eneo la hatari, anaweza kuingia ndani ya 18 badala ya kutafuta kila njia apate nafasi ya kupiga shuti, anageuka tena nyuma kumtafuta mtu mwingine.

Ni kweli kuna makipa nchini ni wazuri wakiwa na mpira miguuni, lakini wanaweza kufanya makosa muda wowote. Na hiyo ni kama watakutana na mastraika jasiri, wenye uchu wa kutaka kufunga mabao, wenye uthubutu na kujituma.

Kama Mane ameweza kwenye uwanja mzuri wa Wembley, je kama mastraika wa Bongo wanafanya kwenye viwanja hivi vya kwetu ambavyo haviko vizuri. Wanachotakiwa ni kuacha uvivu na kufanya mazoezi sana, ili wawe na pumzi na fiziki ya kutosha.

# Vifo vya wanyamapori barabarani vyashtua

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini vifo vya wanyapori 614 kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha mwaka mmoja, sawa na vifo vya wanyamapori 51 mwezi.

CAG Charles Kichere anabainisha takwimu hizo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 aliyoikabidhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 30, mwaka huu kisha kuwasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne iliyopita.

Anasema Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) linasimamia jumla ya hifadhi 22 zenye ukubwa wa kilomita za mraba 104,170. Kati yake, ni Hifadhi za Taifa Mikumi, Serengeti, Tarangire na Ziwa Manyara.

CAG anasema Hifadhi ya Taifa ya Mikumi inapitiwa na barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 45 huku Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ikipitiwa na barabara ya changarawe yenye urefu wa kilomita 12 ikitokea Mbalageti hadi Mto Robana.

"Ukaguzi wangu ulibaini kuwa katika mwaka 2020/21, wanyama 535 waliuawa kwenye ajali za barabarani katika Hifadhi ya Taifa Mikumi kulinganishwa na wanyama 106 katika mwaka 2019/20.

"Idadi hii ni ongezeko la wanyama 429, sawa na asilimia 405. Wakati huohuo, nilibaini kuwa wanyama 50 waliuawa katika Hifadhi ya Taifa Serengeti; wanyama 18 waliuawa katika Hifadhi ya Taifa Tarangire; na wanyama 11 waliuawa katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara.

"Kwa maoni yangu, ikiwa hatua madhubuti za usalama hazitachukuliwa kuzuia uzembe wa madereva ndani ya barabara zinazopita kwenye hifadhi za taifa, kuna uwezekano wa wanyamapori kuendelea kuuawa kwa ajali za barabarani.

"Ninapendekeza serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), ipitie upya taratibu za uendeshaji salama wa magari ndani ya hifadhi za taifa nchini ili kudhibiti ajali zinazoua wanyamapori hifadhini," anatoa hoja.

**UPUNGUFU WA FEDHA**

CAG pia anasema amebaini upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika hifadhi za taifa. Anafafanua kuwa kabla ya mwaka 2020/21, mapato ya utalii yalikuwa yanakusanywa na TANAPA na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), lakini kuanzia Julai Mosi, 2020, serikali iliagiza kisheria mapato hayo yakusanywe na Mamlaka ya Mapato (TRA) huku serikali ikiahidi kutoa fedha zinazohitajika kwa hifadhi hizo kulingana na bajeti za hifadhi hizo.

Hata hivyo, CAG anasema mapitio yake yalibaini tofauti kubwa kati ya bajeti zilizoidhinishwa kwa ajili ya hifadhi hizo na kiasi kilichotolewa na serikali kugharamia miradi ya maendeleo ya hifadhi husika.

"Kwa mfano, NCAA ilitarajia kupokea Sh. bilioni 31.21 kulingana na bajeti yake ya shughuli za maendeleo, lakini serikali ilitoa Sh. bilioni 10.27 tu, sawa na asilimia 33 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hivyo, miradi iliyotekelezwa ilikuwa miradi 15 tu kati ya miradi 36.

"Pia, nilibaini kuwa kiasi hicho cha Sh. bilioni 10.27 kilichelewa kutolewa kwa muda wa miezi saba, ambapo mamlaka iliomba fedha hizo tarehe 21 Oktoba 2020 lakini serikali ilizitoa tarehe 5 Mei 2021.

"Kadhalika, nilibaini kuwa bajeti ya maendeleo ya TANAPA ilikuwa Sh. bilioni 69.52 lakini ni Sh. bilioni 26.51 tu, sawa na asilimia 38 ndiyo ziliidhinishwa kutolewa," anabainisha.

CAG ana angalizo kwamba kutolewa kwa fedha chini ya bajeti kulichangia kutotekelezwa kwa shughuli za maendeleo ya hifadhi zinazohusiana na miundombinu, uhifadhi, na huduma za utalii.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, ACP Allan Bukumbi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio mbalimbali jana.
**PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Uzinduzi filamu Royal Tour ulivyoshamiri Marekani

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, leo anatarajia kuzindua filamu ya Tanzania, The Royal Tour katika jumba la makumbusbo la Guggenheim 89th Avenue jijini New York, nchini Marekani.

Rais Samia aliondoka nchini Aprili 14, mwaka huu kuelekea Marekani kwa ziara ya kikazi mbapo pamoja na mambo mengine anatarajia kuzindua kipindi maalum cha kutangaza utalii wa nchi maarufu kama Tanzania The Royal Tour.

Akitoa taarifa kupitia ukurasa wake wa facebook, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema jana kuwa wapo nchini Marekani kwa ajili ya uzinduzi huo na maandalizi yanaendelea vizuri ambapo zaidi ya watu 300 wakiwamo viongozi mashuhuri wanatarajiwa kuhudhuria hafla hiyo.

"Tayari filamu yetu imeshakuwa na matokeo chanya, wadau mbalimbali ambao walishaona trailer za utangulizi, wameipenda nchi yetu wameanza kuifuatilia, na baadhi ya wadau wa utalii duniani wameomba kuonana naye, kujadiliana naye maeneo ya kuwekeza nchini, lakini jumatatu ndio siku muhimu sana kwenye filamu yetu ya royal tour kwa sababu ndio uzinduzi wa kwanza wa filamu hiyo," alisema Abbas.

Alisema hafla hiyo itasindikizwa na burudani mashuhuri kutoka nchini Tanzania na watu kutoka sekta mbalimbali wanatarajiwa kuhudhuria leo ambapo tarehe 21, mwezi huu utafanyika tena jijini Los Angeles, tarehe 28, Aprili utafanyika jijini Dar es Salaam wakati Mei 7, utafanyika Zanzibar.

Kwa mujibu wa Dk Abbas, filamu hiyo itakuwa na matokeo makubwa kwa sababu imeandaliwa kwa namna ya pekee, ambayo haijawahi kutokea ili kuwavutia wawekezaji, watalii na wengineo wanaopenda kuja kutembelea nchini.

Aliongeza kuwa filamu hiyo pia itaonyeshwa kwenye vyombo vya habari, ikiwamo Luninga, na pia kwenye itawekwa kwenye mitadao ya kijamii ili wale ambao hawakuiona kwenye kumbi basi wapate nafasi ya kuiona na kuwa sehemu ya kuisambaza filamu hiyo ili iwafikie watu wengi .

Wakati huo huo Rais Samia anatarajiwa kuongea na Watanzania na wanadiaspora waishio nchini Marekani Aprili 23, mwaka huu katika ukumbi wa Hoteli ya Marriot jijini Washington Marekani.

# Kituo chajikita uhamasishaji kupata chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni jijini Dar es Salaam, ambacho kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kinachopambana na ukatili wa kijinsia, kimeanza kuhamasisha jamii kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19, kila kinapofanya mikutano yake mbalimbali.

Miongoni mwa mikutano hiyo ni ile ya utoaji wa elimu ya kumiliki simu janja ili kuwezesha wanawake na wasichana kufikia fursa mbalimbali kirahisi katika maeneo yao, zikiwamo za biashara waweze kuinuka kiuchumi.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu wa Kituo hicho, Sada Shifta, baada ya kutoa elimu hiyo kwa baadhi ya viongozi wa vikundi vya wanawake na wasichana wa kata ya Mzinga.

"Kituo chetu hakina fungu la kuhamasisha mambo ya chanjo, lakini inabidi tujiongeze kwa kutumia mikutano yetu ya kawaida kuingiza suala la chanjo ili jamii itambue umuhimu wake na kuchukua hatua," alisema Shifta.

Shifta alisema lengo lao ni kuinusuru jamii kutoka kwenye ukatili wa kijinsia na pia wameona ipo haja ya kuinusuru dhidi ya janga la UVIKO-19 kwa kuhamasisha chanjo ili kila mmoja achukue hatua sahihi.

Mwenyekiti wa Kituo hicho ambacho pia kinaitwa Sauti ya Jamii Kipunguni, Fatma Talib, alisema kimeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kusaidia manusura wa ukatili wa kijinsia.

Aidha Mwenyekiti huyo alisema, Kituo hicho kimepunguza utegemezi na kimefanikiwa kununua jenereta, redio, mahema na viti ambavyo watavitumia katika shughuli zao na kukodisha ili kujiingizia kipato.

"Tunavitumia pia katika mikutano yetu mbalimbali ikiwamo ya kutoa elimu kwa wanawake na wasichana kufikia fursa mbalimbali kirahisi katika maeneo yao, zikiwamo za biashara wainuke kiuchumi,"alisema Fatma.

Alisema, Kituo hicho kinapinga ukatili wa aina zote ukiwamo wa kijinsia, lakini pia kimejitanua na kutoa mafunzo ya kilimo na ushonaji kwa makundi mbalimbali na sasa wanapopata nafasi wanahimiza suala la chanjo.

"Kwa kuwa tunaelimisha wanawake na wasichana kumiliki simu janja ili wafikie fursa mbalimbali kirahisi katika maeneo yao, zikiwamo za biashara wainuke kiuchumi, hatuna budi kuwakumbusha chanjo ya UVIKO-19 ,"alisema.



Mmoja wa wananchi wa Halmashauri ya mji wa Tunduma, akitoa kero dhidi ya madaktari anaowatuhumu kuchati na simu bila kuwahudumia wagonjwa mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, juzi. **PICHA: YASINI IBRAHIM**

# Wakusudia kukutana na Waziri Makamba kupinga uagizaji nguzo umeme nje ya nchi

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

UMOJA wa wafanyabishara wa nguzo za umeme Tanzania (UWANGUTA), wameazimia kukutana na Waziri wa Nishati, January Makamba, wakilenga kuishawishi serikali kusitisha mpango wa kuagiza nguzo hizo kutoka nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Negro Sanga, alisema hayo mjini Mafinga wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa mpango huo kama utatekelezwa utaleta athari kubwa za kiuchumi kwa wawekezaji wa ndani, wazalishaji wa miti ya nguzo, wasafirishaji pamoja na kupoteza ajira za Watanzania wengi.

Alisema kuwa UWANGUTA wameazimia kukutana na Waziri Makamba Aprili 28, wakilenga kuishawishi serikali kusitisha mpango wa kuagiza nguzo hizo kutoka nje ya nchi.

Taarifa ya kuwapo kwa mpango huo iliibuliwa hivi karibuni na Mbunge wa Mafinga Mjini, Cosato Chumi, wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu katika kikao cha Bunge la Bajeti kinachoendelea jijini Dodoma. "Tutaandika andiko la athari zitakazotokea kwa wadau wote wa sekta hii ya uzalishaji wa nguzo za umeme na kuliwasilishwa kwa waziri mwenye dhamana ili lifanyiwe kazi ambaye ameahidi kukutana na wadau wa viwanda na pamoja na ma-suppliers (wasambazaji) mjini Mafinga," alisema.

Sanga alisema sekta ya nguzo nchini ilianza kuimarika na kuchochea uanzishwaji wa viwanda vya nguzo, ongezeko la ajira na mapato ya serikali baada ya serikali ya awamu ya tano Julai 2017 kutangaza kupiga marufuku uagizaji wa nguzo za umeme kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha viwanda vya wazawa. "Sasa tumesikia serikali inarejesha utaratibu wa kununua nguzo kutoka nje ya nchi kwa madai kwamba nguzo zinazozalishwa nchini hazina ubora unaosatahili. Inawezekana ikawa kweli, lakini haiwezi kuwa kweli kwa wazalishaji wote pengine kuna wachache miongoni mwetu ambao wanazalisha nguzo chini ya kiwango," alifafanua.

Katibu wa UWANGUTA, Alex Ngogo, alisema sehemu kubwa ya nguzo zinazozalishwa nchini ni ambazo malighafi yake inavunwa katika shamba la serikali la Sao Hill, mjini Mafinga na katika mashamba ya wananchi ambayo miche ya miti hiyo inauzwa na shamba hilo.

"Kwa mantiki hiyo maana yake ni kwamba serikali inatuuzia wafanyabiashara miti isiyo na ubora wa kutengeneza nguzo na tunajiuliza kama hivyo ndivyo kwanini serikali ifanye hivyo?" Alihoji.

Ngogo alisema katika Wilaya za Mufindi na Kilolo, mkoani Iringa na Njombe kuna viwanda 18 vya kuzalisha nguzo huku gharama ya kuanzisha kiwanda kimoja ikiwa ni zaidi ya Dola za Kimarekani 800,000 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 1.6.

Alisema mpango wa serikali wa kuagiza nguzo hizo toka nje ya nchi kwa madai ya ubora unampa ukakasi, kwa kuwa uzalishaji wake hupitia hatua muhimu za ubora zinazohakikiwa na vyombo mbalimbali vya serikali kabla ya kufikishwa sokoni. Tausi Mbalamwezi na Suzana Kilondo, wafanyabiashara wa nguzo nchini, walilalamika huku wakiomba serikali kuhimiza ubora kwa wawekezaji wake ili kulinda viwanda vya ndani.

Mbalamwezi alisema sehemu ya wafanyabiashara hao waliingia katika sekta hiyo kwa ushawishi wa serikali, wakakopa fedha katika benki, wakanunua mitambo na kuanza uzalishaji, na kutoa tahadhari kama wakisitisha huduma hiyo athari yake itakuwa mbaya.

# Malalamiko ya wakulima dhidi ya wafugaji Kwala yatafutiwa dawa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

OFISA Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, Ombeni Msangi, amesema malalamiko ya wakulima dhidi ya baadhi ya wafugaji kuendelea kuwa kikwazo katika shughuli za kilimo Kata ya Kwala yanashughulikiwa kwa kuwaondoa wanaolisha mifugo ya wakulima.

Msangi alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu ambapo alikiri kuwa na taarifa za wananchi hao na kusema kuwa Serikali inashughulikia kero hiyo.

Alisema katika maeneo ya umwagiliaji sheria zinatakiwa kufanya kazi kwa yeyote atakayebainika kulisha mifugo yake kwenye skimu ya umwagiliaji ili kukomesha hali hiyo na uharibifu kwenye mazao.

"Hili suala la malalamiko ya wakulima halijaanza kushughulikiwa leo ni karibu miaka miwili sasa linashughulikiwa ila mambo haya ya kuhamisha watu hasa kipindi cha kiangazi ilikuwa ni shida kidogo kutekelezwa kutokana na hali ya hewa, lakini Serikali inaendelea kulifanyia kazi kwa kudhibiti wafugaji wanaoingia kwenye maeneo kinyemela," alisema.

Akizungumzia suala la wafugaji wapya kwenye maeneo ya wakulima, alisema mwenyekiti wa kijiji na mtendaji wa kata wanafahamu ni mfugaji gani ambaye ameingia kinyemela na kusababisha matatizo kwa wananchi na wanatakiwa kutoa ushirikiano kwenye mamlaka husika ili walioingia kinyume na taratibu waondolewe.

Alisema wafugaji wanaoishi na wakulima wanatakiwa kufuata taratibu kwa kutolisha mifugo yao kwenye mashamba na kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Hivi karibuni Nipashe iliandika habari kuhusu baadhi ya wakazi wa Kwala wanaojihusisha na kilimo kushindwa kufanya shughuli zao kwa kuhofia mifugo ambayo imekuwa ikiharibu mazao mara kwa mara.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Sara Msafiri, aliahidi kushughulikia malalamiko ya wakulima.

# Msukumo unahitajika kudhibiti joto duniani

**Na Jenifer Gilla**

IMEBAKI miaka mitatu kufikia ukomo wa makubaliano ya Paris ambayo pamoja na mambo mengine mataifa yalikubaliana kudhibiti joto ili lisizidi nyuzijoto 1.5 juu ya usawa wa bahari kufikia mwaka 2025.

Ripoti ya jopo la wanasayansi linalochunguza athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa (IPCC), inaonesha kunahitajika hali ya dharura ili kudhibiti joto lisiongezeke kufikia nyuzijoto 1.5 juu ya usawa wa bahari na ikishindikana basi joto linaweza kufika nyuzijoto tatu.

Nipashe ilizungumza na wataalam na wadau wa mazingira hasa mabadiliko ya tabianchi, kama suala hilo litafanikiwa kufikia 2025 na nini kifanyike ili kuongeza msukumo.

Ofisa Mazingira Mwandamizi kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Fedrick Mulinda, alisema mkutano mkubwa wa mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Novemba, mwaka jana, maarufu kama COP 26, haukuridhishwa na mikakati ya nchi tajiri ya kupunguza uzalishwaji wa gesi joto kama zilizokubaliana katika Makubaliano ya Paris mwaka 2010.

"Nchi zenye viwanda vinavyozalisha gesi joto kwa wingi ziliambiwa zipeleke Nationally Determined contributions (NDC's) (Ripoti za mikakati ya kupunguza uzwalishwaji wa gesi joto) kuelezea jinsi watakavyopunguza uzalishaji huo ili kudhibiti joto kuongezeka.

Mwaka jana baada ya ripoti zao kupitiwa ilionekana haijitoshelezi kupunguza joto gesi na hivyo waipitie upya, kwa hiyo utaona hapo jinsi hali ilivyo ngumu kufikia lengo hilo," alisema Mulinda.

Alisema kupitia mkutano huo ilionekana kuwa kama nchi tajiri zikifuata mipango iliyowasilisha katika kupunguza uzalishaji wa gesi joto itasababisha joto kuongezeka hadi kufikia nyuzijoto 2.7. alisema.

Alisema kwa mantiki hiyo kufanikiwa au kutofanikiwa kwa malengo ya kudhibiti joto kunategemea mipango ya nchi tajiri kwa kuwa ndiyo wazalishaji wakubwa wa gesi joto na kushindwa kwao kutasababisha hali kuendelea kuwa mbaya na hata lekuondoa kabisa uzalishaji wa hewa chafu (zero emission) kufikia mwaka 2050 hautofanikiwa. Mwanaharakati wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Kibona Gharama, alisema kuwa mpango hautofanikiwa kwa 2025 kwa sababu utekelezaji wa vipaumbele vya taifa (NDCs) umebaki kwenye makaratasi kuliko uhalisia.

Jamii pia haina uelewa wa kutosha kuhusu vipaumbele hivyo na kwa namna gani wanatakiwa kuchangia katika kuvifikia, lakini pia nchi maskini hazijawezeshwa ipasavyo kutoa elimu ya kutosha kwa jamii kuhusu athari za mabadiliko ya hali hewa.

Naye Ofisa Mradi kutoka Taasisi ya Tanzania Cleanup and Conservation Initiavitive (TCCI), Frowin Yustinia, alisema suala la kufanikiwa au kutofanikiwa yote hutokana na wale wa lioafikiana hasa nchi tajiri ambazo wao ndiyo wanahamasisha upunguzaji wa nishati za gesi joto, lakini wao ndiyo wazalishaji wakubwa.

"Mfano unaona hata vita vinavyoendelea pia ni matumizi ya silaha za moto yote yanaathiri tabianchi, wao kwa wao ndiyo wanapigana na ndiyo mahasimu wakubwa katika hii vita, lakini bado wao ndiyo walikaa kwenye Paris Agreement kukubaliana upunguzaji wa gesi," alisema.

Mkurugenzi wa kampuni ya mazingira ya HUDEFO, Sara Pima, alisema kwa mujibu wa ripoti ikiwamo ya IPCC iliyotolewa hivi karibuni suala la kudhibiti joto hilo linaonekana bado ni kitendawili ikizingatiwa kuwa kumebaki muda mchache.

Alisema kinachotakiwa ni nchi maskini ikiwamo Tanzania ziwe na mikakati ya kujijengea uhimilivu wa hali hiyo ikiwamo upandaji wa miti ya kutosha kwa sababu zenyewe zinachangia kwa kiasi kidogo sana (asilimia 0.4) katika kuzalisha gesi joto, lakini madhara yake ni makubwa.

HABARI KITAIFA

# NMB yataka upendo baada ya Ramadhani

**Na Jenifer Gilla**

BENKI ya NMB imefuturisha Waumini wa Kiislamu jijini Dar es Salaam, huku ikiwakumbusha kuutumia Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kufanya tafakari juu ya maadili yanayounganisha jamii, upendo kwa familia zao, shukrani kwa Mungu, kufanya toba za dhati na ushiriki endelevu wa ibada hata baada ya mfungo.

Wito huo umetolewa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, wakati wa hafla hiyo iliyofanyika Serena Hoteli na kuhudhuriwa na waumini hao, viongozi wa dini, Serikali na wageni waalikwa, akiwamo Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Aboubakary Zubery Ally Mponzi alisema kipindi cha mfungo wa Ramadhani, ni wakati sahihi kwa Waislamu na jamii kwa ujumla kutafakari juu ya maadili yanayotuunganisha binaadamu wote, upendo kwa familia zetu, shukrani kwa Mungu, kufanya toba za dhati na ushiriki endelevu wa ibada.

"Kwa hiyo huu ni mwezi muhimu kwa Waislamu na kwa jamii kwa ujumla, nasi NMB tunakitumia kipindi hiki kujumuika na wateja wetu, kwa sababu tunaamini jamii zetu hustawishwa kwa swala na toba za dhati zinazotolewa wakati huu," alisema. Mponzi aliongeza kuwa Mwezi wa Ramadhani ni baraka kwa maisha ya watu wengi na taifa kwa ujumla, huku akimshukuru Sheikh Mkuu, viongozi wa dini na Serikali, wateja na wafanyakazi wa benki hiyo kwa kutumia muda wao kujumuika katika hafla hiyo, ambayo haikufanyika kwa miaka miwili kutokana na mkwamo wa UVIKO 19.

"Nawatakia Ramadhani njema na mkawe na mwisho mwema wa mfungo, NMB tunatoa wito kwenu kwamba baada ya mfungo, ibada na wema uendelee, kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kupata thawabu na kujenga jamii yenye upendo na amani," alisema Mponzi.

Naye, Mufti wa Tanzania, Aboubakary Zubery, aliushukuru uongozi wa NMB na kuupongeza kwa kile alichokiita 'Moyo wa Kuthamini na Kujali,' uliowafanya waone umuhimu wa kukutanisha waumini wa dini ya Kiislamu na kuwafanyia moja kati ya Furaha Mbili za Mfungaji wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani zilizotajwana Mtume Muhammad (S.A.W).

"Mtume Muhammad (S.A.W) amesema: Mwenye Kufunga Ramadhani huwa na nyakati mbili za furaha. Furaha ya kwanza ni pale anapohitimisha funga ya siku wakati wa kufuturu jioni na furaha ya pili ni wakati wa kuingia kwake peponi kutokana na kukubaliwa kwa ibada hiyo.

"Sasa hii furaha ya kwanza ambayo nyinyi mmeijaalia hadi sisi kukutanishwa hapa, mnastahiki kupongezwa na mnastahili kuonwa kuwa mna tabia nzuri. Viongozi wa NMB mmeonesha tabia njema ya 'Kuthamini na Kujali, Mungu awabariki.

"Msingekuwa na Moyo wa Kuthamini na Kujali, msingeona umuhimu wa kukusanya watu kuwafuturisha. Futari hii ina maana kubwa sana, inajenga undugu, inakutanisha watu waliopotezana, pia inaondoa mafundo nyoyoni mwa walioalikwa, lakini pia watu wanafurahi kwa kule kufuturishwa. Meneja wa NMB, Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, aliwashukuru Waumini wa Kiislamu, Viongozi wa Dini, Serikali na wageni waalikwa waliohudhuria hafla hiyo, kwa kuwa kwani wangeweza kwenda kupata futari kwingine, hasa majumbani, lakini wakatumia muda ambao ni rasirimali muhimu, kuungana na NMB.

# Pemba walia kupaa bei ya vyakula

**NA MWANDISHI WETU**, PEMBA

WAKAZI kisiwani Pemba wamelalamikia kuongezeka kwa bei za vyakula katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, jambo ambalo linasababisha wasio na uwezo kushindwa kumudu kununua.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi wa wilaya za Mkoani na Wete walisema kuwa, wafanyabiashara wanakosa imani hata kipindi hiki.

Walisema kuwa, kila ifikapo Mwezi Mtukufu wa Ramadhani bidhaa zote hupandishwa bei, jambo ambalo linawaumiza wananchi hasa wenye kipato cha chini, kwani wanashindwa kununua.

"Ramadhani ni mwezi wa kuchuma mema, lakini wafanyabiashara wanachuma dhambi kwani vitu vingine hakuna sababu ya kuongeza bei, lakini wanafanya makusudi, wawafikirie wasio na uwezo, wajane na mayatima", alisema mmoja wa wakazi hao.

Mkazi wa Mkoani, Said Abdalla Mohamed, alisema bidhaa zote kama muhogo, ndizi, magimbi, nazi, mafuta ya kula na samaki zimepanda bei ukilinganisha na kabla ya Ramadhani kiasi ambacho wanashindwa kununua.

"Kabla ya Ramadhani nazi tulinunua mpaka shilingi 600, lakini kipindi hiki tunanunua nazi moja kwa shilingi 1200, kwa kweli ni mtihani kwetu kwa sababu kila inapofika mwezi huu wafanyabiashara na wakulima wanatukomoa, alisema.

Aliwaomba wafanyabiashara wapunguze bei za vyakula ili wananchi waweze kumudu futari sambamba na kuiomba Serikali ifuatilie kuhakikisha kwamba bei za bidhaa zinakuwa nafuu.

Zubeir Mohamed Jecha alieleza kuwa kawaida yake ni kwenda sokoni kununua bidhaa mbalimbali kwa ajili ya futari, lakini ameona mabadiliko ya ongezeko la bei za bidhaa katika kipindi cha Ramadhani.

"Kwa kweli kila ifikapo Mwezi wa Ramadhan wafanyabiashara huwa na kawaida ya kupandisha bei za bidhaa, tunaomba wapunguze ili wapate fungu kwa Allah (Subhanahu Wataala)," alisema.

Mkazi wa Chasasa Wete, Asha Khamis Abdalla, alisema kuwa juzi alipata mshangao baada ya kufika dukani na kupewa bei ya mafuta ya kula, ambapo alishindwa kununua vitu vingine alivyokusudia.

"Kama ingekuwa sina ulazima ningeyasamehe, kwa sababu nilipeleka pesa ili nipate na vitu vingine ,lakini niliambiwa nusu chupa ni shilingi 2,500 kwa hali hii wengine tutashindwa futari,", alisikitika alilalamika.

Khadija Mohamed Ali, mkazi wa Chasasa, alisema wafanyabiashara wamekuwa wakipandisha bei za bidhaa kiholela, hivyo ipo haja kwa Serikali kuliangalia kwa kina jambo hilo na kulitolea ufafanuzi.

Muuza duka ambae hakutaka kutaja jina alake, mkaazi wa Wete, alisema wanaongeza bei kulingana na bei wanayonunulia bidhaa na kueleza kwamba kila kitu kimeongezeka bei kwa zaidi ya miezi miwili nyuma.

Mfanyabiashara wa nazi katika soko la Mkoani, Asha Othman Kombo, alisema bei ya nazi iko chini katika kipindi hiki ukilinganisha na kabla ya Ramadhani, kwani walikuwa wanauza nazi shilingi 1,000, lakini kwa sasa ni kuanzia 800 hadi 500.

Mfanyabiashara wa muhogo Sheha Khatib ambaye pia ni mkaazi wa Kiwani Mkoani, alisema kuwa yeye hakupandisha bei ya bidhaa hiyo na anauza fungu shilingi 2,000 kabla ya Ramadhani na mpaka sasa.

Karani wa diko la Mkoani, Abdalla Ali Baka,r alisema katika kipindi hiki samaki ni wengi, lakini ni ghali sana kwa sababu wengine huchuma dhambi katika Mwezi wa Ramadhani na ndio wanaongeza bei.



Mbunge wa Jimbo la Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma (kushoto), akizungumza na vijana na viongozi baada ya kuwakabidhi pikipiki mpya za mkopo wa asilimia 10 ya halmashauri, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vigwaza wapaza sauti kilio cha maji

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

WAKAZI wa Kwedihungo Kata ya Vigwaza wilayani Chalinze Mkoa wa Pwani, wameiomba Serikali kuwaweka kwenye mipango ya kusambaziwa maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA) kuondokana na adha wanayokumbana nayo kwa sasa.

Wakizungumza na Nipashe jana, walisema kwa sasa wanalazimika kununua dumu la maji la lita 20 kwa Sh.500, hali ambayo inawafanya baadhi yao wanashindwa kumudu gharama hizo.

Juma Mlasa aliliambia Nipashe kuwa maji kwao yamekuwa kikwazo katika shughuli zao za maendeleo kutokana na kutumia muda na gharama kuyapata ambayo hata hivyo hayakidhi mahitaji.

Juma alisema wanawake wa kijiji hicho wanalazimika kutembea zaidi ya kilometa nne kwenda kufuata maji katika kituo(kioski) ambacho kipo katika eneo la Buyuni.

Marlian Ismail, mkazi wa Kwedihungo, alisema tatizo la maji wamekuwa wakiliwasilisha kwa viongozi wao mara kwa mara, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi kwani hadi sasa wanayafuata mbali na wanapoishi.

"Wananchi wa kitongoji chetu maisha yao ni hali ya chini na hivyo wengi wao kushindwa kumudu gharama za kununua maji kila siku," alisema.

Kwa mujibu wa Marlian, wako wananchi wanaolazimika kutumia maji ya bwawa ambayo si salama, lakini wanalazimika kufanya hivyo kutokana na umbali wa kupata maji ya bomba.

Machi 22, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassani alizindua mradi wa maji wa Mlandizi -Mboga ambao ambao umejengwa na DAWASA ukiwa na vituo viwili vikubwa cha Msoga na kingine Vigwaza.

Akiwa katika uzinduzi huo alielekeza DAWASA kupatiwa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kusambaza maji kwa wananchi kupunguza kero iliyopo ya kufuata maji kwenye vituo (vioski) ambavyo vingine viko mbali na makazi ya watu.

## Kesi 42 udhalilishaji zaripotiwa Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya kesi 42 za vitendo vya udhalilishaji zimeripotiwa katika Ofisi ya Naibu Mrajisi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Kisiwani Pemba kwa mwaka 2021.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Chake Chake, Naibu Mrajisi huyo, Hidaya Omar Khamis, alisema kuwa bado tatizo la udhalilishaji kwa wanafunzi lipo na ni changamoto kubwa.

Mrajisi huyo alieleza kuwa kesi ambazo ziliripotiwa katika ofisi yao ni pamoja na ubakaji, mimba kwa wanafunzi, udhalilishaji pamoja na kulawitiwa ambapo jumla ya matukio hayo ni 42.

"Kwa upande wa Wilaya ya Wete, kesi ambazo ziliripotiwa ofisini kwetu ni (11), ambapo kesi za udhalilishaji zilikuwa (4), ubakaji (2), udhalilishaji (4), mimba (1) huku kesi za ndoa ikiwa hamna,"alieleza.

Sambamba na hayo naibu huyo alieleza kuwa kwa upande wa Wilaya ya Micheweni kesi ambazo ziliripotiwa ni (10) ikiwa ni kesi ya ndoa (1), mimba (8), ulawiti (1) huku vitendo vya udhalilishaji na ubakaji ikiwa hamna.

"Ama kwa upande wa Wilaya ya Chake Chake, Naibu Mrajisi alieleza kuwa kesi zilizoripotiwa ni (10), ambapo kesi za udhalilishaji ni (1), ubakaji (2), mimba (5), ulawiti (1) huku kesi ya ndoa ni (1)".

Kwa upande wa Wilaya ya Mkoani, kesi ambazo tulizipata ni kesi (11), ambao kesi za ubakaji ni (4), kesi za ulawiti ni (1), udhalilishaji (2), mimba (4) huku kesi za ndoa ikiwa hamna," alisema Naibu Mrajisi.

Aidha Mrajisi Hidaya alibainisha kuwa changamoto kubwa ambayo wanakabiliana nayo ni wazazi kuwaoza watoto wao wa kike kwa siri .

Aidha kwa wale ambao kwa bahati mbaya wanaopata ujauzito (mimba) wakati bado ni wanafunzi, wanapojifungua (wanapozaa) hukataa kurudi tena.

"Changamoto kubwa ambayo tunayo ni wazazi kuwaozesha waume watoto wa kike wakati bado ni wanafunzi, lakini pia wale ambao kwa bahati mbaya walipata ujauzito (mimba) wakati bado wanasoma, hutakiwa kurudi tena skuli kuendelea na masomo yao lakini hukataa kufanya hivyo, " alisema Hidaya.

Naibu Mrajisi Hidaya alitoa wito kwa wazazi na walezi kushirikiana pamoja ili kutokomeza vitendo vya udhalilishaji ambavyo bado ni hatari sana kwa jamii.

# Kanisa Anglikana lawaanzishia miradi vijana mitaani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Morogoro, limefanikiwa kuyashawishi makundi ya vijana yaliyokuwa mitaani kwenye vijiji vya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro na kuyapeleka kuanzisha miradi ya kufanya shughuli za kilimo na ufugaji wa kisasa ili kujikwamua kiuchumi.

Ushawishi huo umefanywa na kanisa hilo kupitia mradi wa uwezeshaji wa kiuchumi unaostahimili mabadiliko ya tabianchi kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Makanisa ya Watu wa Norway (NCA-Tanzania).

Ofisa mradi wa kuhimili Mabadiliko ya Tabia Nchi na Uwajibikaji wa Wananchi (CSEE) kutoka Kanisa la Anglikana, Pius Ng'irwa, alisema hayo wakati akizungumza katika mdahalo uliohusisha viongozi wa serikali za vijiji hivyo vinavyopitiwa na mradi, viongozi wa dini, halmashauri na wadau wa taasisi mbalimbali.

Ng'irwa, alisema vijana hao wamejitokeza baada ya kupewa elimu za kuanzisha shughuli za kilimo cha mboga na matunda, ufugaji wa kuku wa kisasa, kuunda vikundi vya huduma ndogo za kifedha na kutumia teknolojia za kisasa katika kupata taarifa mbalimbali za kilimo.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwaondoa vijana wanaokaa vijiweni na kwenye barabara kuu wakifanya shughuli zisizo halali na badala yake wajikite katika kilimo cha kisasa kinachoendana na mabadiliko ya tabianchi na ufugaji ili kujipatia kipato.

Hata hivyo, Ng'irwa, alisema pamoja na kundi hilo la vijana kuhamasika kufanya shughuli hizo, lakini ipo changamoto ya kukosekana kwa ardhi katika vijiji vya mradi kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo na kukwamisha utekelezaji huo.

"Tayari zipo taasisi kama NSSF, kampuni za mbegu zimejitokeza kuwasaidia haya makundi ya vijana walihamasika kufanya shughuli za kilimo na ufugaji, lakini wanachotaka wamilikishwe ardhi yao, hivyo tunaomba Serikali ya Wilaya ya Kilosa kusaidia upatikanaji wake," alisema Ng'irwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mfulu kilichopo wilayani Kilosa, Luka Chitete, alisema katika kijiji hicho kuna makundi ya vijana yamejitokeza kufanya shughuli za kilimo na ufugaji, lakini tatizo ni ukosefu wa ardhi licha ya kuwaslisha ombi lao kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, mpaka sasa hawajapatiwa majibu.

"Yamejitokeza makundi mengi ya vijana baada ya mradi wa CSEE kutoa elimu kwao, lakini kuna tatizo la upatikanaji wa ardhi mashamba mengi ni ya wawekezaji na yapo yaliyofutwa tumejaribu kuomba kwa halmashauri mpaka sasa hatujapatiwa majibu," alisema.

Naye Ofisa Teknolojia wa mradi wa uwezeshaji wananchi na uwajibikaji kutoka CSEE, Mathias Sanane, alisema tayari wameshaunda vikundi 41 kati yao vya vijana ni 26 katika vijiji vya mradi ikiwamo, Kisanga, Zombe, Kasiki, Mfulu, Kitete, Dumila, Mbigili, Magole na muitikio mkubwa wa kufanya shughuli hizo za kilimo na ufugaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Kisena Mabuba, alilipongeza Kanisa la Anglikana kuja na mradi huo wa kuwasaidia vijana kujiajiri ili kujipatia kipato kupitia shughuli za kilimo na ufugaji.

Ili kuondoa kikwazo cha upatikanaji wa ardhi, aliagiza kila kijiji kuanzisha maeneo na kuwamilikisha kundi la vijana ili kutekeleza mradi huo huku akiahidi kutoa kipaumbele kwa kundi lolote la vijana kugaiwa mashamba yaliyokuwa ya wawekezaji katika wilaya hiyo na kufutwa umiliki wake na kurudishwa serikalini.



Mtaalamu wa uchumi ambaye pia ni mwalimu wa neno la Mungu, Mgisa Mtebe, akifundisha waamini wa Kanisa Anglikana, Parishi ya St. James Arusha, Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, katika kongamano la Pasaka lililobeba ujumbe wa uwezo wa damu ya Yesu katika kukomboa uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa siku 10. **PICHA: WOINDE SHIZZA.**

# RC Kunenge alipa 'meno' baraza la ardhi Bagamoyo

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka wajumbe wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani kufanya kazi kwa weledi bila kumuogopa mtu, kwani hakuna aliye juu ya sheria.

Aidha, ametaka kusimamiwa maadili katika utendaji kazi wao kwa kuondoa migogoro ya ardhi kwa wakati, kuondoa ugumu ambao unaweza kutokea endapo mashauri yatachelewa.

Kunenge alitoa maelekezo hayo mjini Bagamoyo alipokuwa akiwaapisha wajumbe wa baraza hilo, ambapo alisema hatarajii kusikia wajumbe hao wameshindwa kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

"Visitokee vikundi vinawatisha kwenye kazi zenu, msiogope vitisho, tendeni haki bila kumuogopa mtu yeyote wala kufanya upendeleo katika majukumu yenu nitawaunga mkono," alisisitiza Kunenge.

Alisema katika utawala wa sheria hakuna aliye juu ya sheria, hivyo wajumbe walioapishwa wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia ufahamu, ujuzi na utaalamu na kuishi kulingana na majukumu yao.

" Mimi sitawauliza juu ya utendaji wenu, nitajua ufanisi wenu au hakuna ni kwa kiwango gani mtatatua changamoto kwa jamii inayowazunguka na niwaambie hatutarajii tuwe na watu ambao hawatakuwa msaada, ikifikia hali hiyo tutawabadilisha," alisema Kunenge.

Alisema atasikitika endapo maamuzi yanayotolewa na baraza hilo asilimia kubwa yakaonekana ni batili

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Abdallah, alimpongeza mkuu wa mkoa kwa kuwaapisha wajumbe hao ambapo alisema kukosekana kwa baraza hilo ilikuwa kero kwa wananchi ambao walikuwa wanalazimika kwenda Kibaha kufuatilia mashauri yao.

Zainabu alisema kuwapo kwa baraza hilo kutasaidia kupunguza kero za migogoro ya ardhi iliyokuwapo kwani kero za wilaya hizo anazopokea mara kwa mara asilimia 60 ni za migogoro ya ardhi.

"Zaidi ya miaka kumi mabaraza yameundwa, lakini Bagamoyo ilikuwa bado na hiki kilikuwa kilio kikubwa kwa wananchi wetu sasa kupitia kwa mkuu wetu wa mkoa ufumbuzi umepatikana," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kibaha, Sara Mbuga ambaye alimwakilisha Msajili wa Mabaraza ya Ardhi mikoa ya Pwani na Dar es Salam, aliwataka wajumbe walioapishwa kufanya kazi kwa uadilifu.

Nipashe
Spotika




MCHEZAJI MUHIMU ZAIDI KWA KILA TIMU 6-BORA EPL UK. 12-13



KARIM BENZEMA

# WAKALI WA NYAVU WENYE MCHANGO WA MABAO 30

**LONDON,** England

KUMEKUWA na soka la kufurahisha hadi sasa katika msimu wa 2021-22. Wakati baadhi ya wachezaji wakifanya vema katika safu ya ulinzi ya mchezo huo, washambuliaji nao wamecheza soka ya hali ya juu. Washambuliaji wachache wa katikati, haswa, wamekuwa wa kufurahisha sana msimu huu.

Mabao ni muhimu katika mchezo wowote, lakini kuna baadhi ya wachezaji wanaofunga wiki baada ya wiki kwa upande wao. Wanacheza kwa kiwango cha juu katika kila mchezo na mara nyingi huthibitisha kuwa watengenezaji tofauti kwa pande zao.

Kuchangia hata mabao 20 kwa msimu bado ni ndoto kwa wachezaji kadhaa. Kwa hivyo, mtu yeyote anayeweza kuchangia mabao 30 ni hazina kubwa kwa upande wa timu. Kwa maelezo hayo, tuwatazame wachezaji wanne ambao wamehusika katika mabao 30 msimu huu (2021-22), twende sasa...

Kumbuka: Ni ligi tano bora pekee barani Ulaya ndizo zimezingatiwa katika makala haya.

### #4. KYLIAN MBAPPE - 30

Kylian Mbappe, mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kwenye orodha hii, amekuwa mzuri tena msimu huu. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, bila shaka ndiye winga tishio zaidi katika soka la Ulaya kwa sasa.

Mbappe ambaye tayari ni mshindi wa Kombe la Dunia, anaweza kubadilisha kasi na kuwashinda mabeki kupitia ustadi na kasi yake. Uamuzi wake katika nafasi tatu za mwisho ni mzuri pia. Kwa hisani yake, nyota huyo wa Paris Saint-German ana mabao 17 na asisti 13 kwenye Ligue 1 msimu huu.

Mmoja wa washambuliaji bora wa pembeni katika soka la dunia, Mbappe anatazamiwa kuwa na ubora katika kipindi chote cha maisha yake ya soka. Nyota huyo wa Ufaransa pia alifanikiwa kuhusika kwa mabao 30 msimu uliopita.

### #3. MOHAMED SALAH - 30

Mohamed Salah raia wa Misri amepata huzuni nyingi kwenye hatua ya kimataifa katika kipindi cha miezi kadhaa iliyopita akiwa na timu ya taifa. Alishindwa na Senegal katika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika na akashindwa kufuzu kwenye michuano ya Kombe la Dunia la 2022 dhidi ya timu hiyo hiyo.

Ingawa yeye si mshambuliaji wa kati, Salah ndiye mfungaji bora wa mabao kwa Liverpool. Mkali huyo wa Kiafrika amefanya vema chini ya mfumo wa kocha, Jurgen Klopp na msimu huu umekuwa tofauti.

Amefunga mabao karibu katika kila mechi, huku akitoa pasi ya bao dhidi ya timu anazoshindwa kuzifunga. Amefunga mabao 20 na kutoa asisti 10 katika mechi 28 za Ligi Kuu England hadi sasa.

Utimamu wa Salah pia ni wa kupongezwa na anaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuisaidia Liverpool kufukuzia Manchester City kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

### #2. ROBERT LEWANDOWSKI - 32

Robert Lewandowski amekuwa kitovu cha ubabe wa Bayern Munich kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. Mshambuliaji huyo wa Poland alivunja rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja mwaka jana (41) na anaendelea na kasi ile ile msimu huu.

Bavaria hao wanaweza kunyakua taji lingine la ligi baada ya ushindi mara nne kati ya michezo sita iliyopita. Wanaongoza kwa pointi 13 kileleni mwa msimamo dhidi ya Borussia Dortmund walio nafasi ya pili.

Lewandowski amekuwa na jukumu muhimu katika mafanikio ya Bayern mwaka huu tena. Amefunga mabao 31 na kutoa asisti moja katika mechi 28 za Bundesliga.

Kilichovutia zaidi ni uchezaji wake wa pande zote. Ingawa amesajili pasi ya bao moja pekee, amerahisisha uchezaji.

Zaidi ya hayo, huku kukiwa na mechi sita za ligi kuchezwa, Lewandowski anaweza kuvuka mabao 40 msimu huu.

### #1. KARIM BENZEMA - 35

Karim Benzema amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Real Madrid tangu Cristiano Ronaldo alipoondoka kwenda Juventus mwaka 2018. Ametwaa kijiti hicho kwa ustadi na amekuwa mchezaji muhimu sana kwa 'Los Blancos' msimu baada ya msimu.

Shujaa mkubwa kabisa kwa washindi mara 13 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Benzema huwa katika harakati kali. Daima anatafuta kutumia nafasi yoyote na kufunga bao kwa upande wake. Vile vile, ikiwa anatatizika mbele ya goli, anajaribu na kuwaweka wachezaji wenzake. Daima yuko kwenye mchanganyiko na Madrid italazimika kumshukuru ikiwa watatwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu.

Ili kuweka wazi umuhimu wake, kati ya mabao 61 ya Real Madrid kwenye ligi msimu huu, Benzema amechangia mabao 35. Mabao yake 24 na asisti 11 ni zaidi ya asilimia 50 ya mchango wake kwa timu.

## ISIKUPITE

NCHI tano zilizoshiriki mara nyingi zaidi Kombe la Dunia tangu lianzishwe mwaka 1930 ni Brazil (mara 22), Ujerumani (20), Italia (18), Argentina (18) na Mexico (17).



# MCHEZAJI MUHIMU ZAIDI KWA KILA TIMU 6-BORA EPL



BRUNO FERNANDES

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England ndio mashindano ya Klabu yanayofuatiliwa zaidi duniani. Ligi ya Daraja la Kwanza ya England inajulikana kwa mechi zake za kusisimua, ambazo huwa hazikosi kuwaburudisha mashabiki.

**Kutokana na hilo, Klabu za Ligi Kuu England ni moja ya timu tajiri zaidi duniani. Mapato mengi wanayopata kupitia mikataba ya utangazaji ni kubwa kuliko yale ambayo pande zingine kadhaa za Ulaya hupata kwa msimu.**

Kwa sababu ya nguvu zao za kifedha, timu hizi pia zina uwezo wa kunyakua baadhi ya wachezaji bora kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Manchester City, Chelsea, Liverpool, Manchester United, Arsenal na Tottenham Hotspur zinajulikana sana kama timu sita bora za Ligi Kuu England.

Timu hizi zimejaa nyota ambao wana uwezo mkubwa na uwezo wa kubadili matokeo uwanjani.

Leo, tunatazama mchezaji mmoja kutoka katika klabu hizi sita ambaye ni muhimu sana kwa timu yake, haya sasa...

### #6. TOTTENHAM HOTSPUR - SON HEUNG-MIN

Son Heung-Min ni mmoja wa wanasoka wanaopendwa zaidi duniani. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini ni straika wa kiwango cha kimataifa ambaye amekuwa akicheza kwa kiwango cha juu sana pale Spurs tangu ajiunge nayo kutoka Bayer Leverkusen mwaka 2015.

Pamoja na kelele zote kuhusu mustakabali wa Harry Kane na kulazimisha Spurs kuwa chini ya uchunguzi katika wiki za mwanzo za msimu, ni Son ndiye aliyeibeba timu. Kiwango cha Kane kilitetereka sana kutokana na kelele zilizokuwa zikimzunguka, lakini Son aliweka kichwa chini na kufanya vile alivyoweza kwa upande wake katika kipindi kigumu.

Alionesha na kufuta dhana kwamba Tottenham ni timu inayomtegemea mtu mmoja tu, Kane. Katika mechi 33 kwenye michuano yote kwa Spurs, Son amefunga mabao 12 na kutoa asisti saba.

Kwa sasa yeye ni mchezaji muhimu kwa Tottenham na ni kipenzi cha mashabiki.

### #5. ARSENAL - BUKAYO SAKA

Bukayo Saka alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Arsenal katika msimu wa 2020-21. Kinda huyo ni ishara ya juhudi za 'Washikabunduki' hao kuzalisha vipaji bora ambavyo vinaweza kucheza moja kwa moja na wachezaji waliobarikiwa zaidi kiufundi kwenye mchezo huo.

Saka alikosolewa sana kwa kukosa penalti muhimu wakati England ilipopoteza kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Italia katika fainali ya Euro 2020. Ingawa alitatizika wiki za mwanzo za msimu wa 2020-21, Saka anaonekana kurejea kwenye kiwango chake.

Uelekevu wake na ustadi wake huwapa Arsenal makali kila wanapopiga hatua mbele. Saka siku zote anaonekana kama mchezaji ambaye ana uwezekano mkubwa wa kuleta mabadiliko katika safu ya ushambuliaji ya Arsenal.

Katika mechi 30 kwenye michuano yote kwa 'Washikabunduki' hao hadi sasa msimu huu, Saka amefunga mabao tisa na kutoa asisti tano.

### #4. MANCHESTER UNITED - BRUNO FERNANDES

Bruno mchezaji wa kimataifa wa Ureno ni miongoni mwa wachezaji wachache sana wenye uwezo wa kuleta mabadiliko katika kila mchezo anaocheza.

Fernandes anashika nafasi ya kwanza pamoja na Trent Alexander-Arnold na Mohamed Salah kwa nafasi nyingi zaidi walizotengeneza kwenye Ligi Kuu (14 kila mmoja). Mchezaji huyo hajawa na msimu mzuri kwa kiwango chake kwa sasa.

Bado amefunga mabao tisa na kutoa pasi za mabao 14 katika mechi 36 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao kufikia sasa msimu huu. Namba hizo zingekuwa bora zaidi ikiwa washambuliaji wa Manchester United ambao hawakufanya vizuri wangeweka kando idadi kubwa ya nafasi ambazo Fernandes ametengeneza.

### #3. CHELSEA - MASON MOUNT

Chelsea ni timu ambayo inatisha sana katika safu ya ulinzi. Shida zao mara nyingi hutoka kwenye upande wa kushambulia. Si Timo Werner wala Romelu Lukaku ambaye amethibitisha kuwa aina ya mshambuliaji ambaye wamekuwa wakimtafuta.

Mason Mount mchezaji mwenye umri wa miaka 23 ni kiungo mkabaji wa hali ya juu ambaye huwa hashindwi kufanya jambo zuri awapo uwanjani.

Kasi, akili na maamuzi ya Mount katika robo tatu ya mwisho imeisaidia Chelsea mara kwa mara kuwashinda wapinzani wao.

Katika mechi 37 kwenye michuano yote, aliyoichezea Chelsea hadi sasa msimu huu, Mount amefunga mabao saba na kutoa asisti nane.

### #2. LIVERPOOL - VIRGIL VAN DIJK

Swali la wazi hapa ni, kwa nini Mohamed Salah hatajwi mbele ya Virgil van Dijk? Bila shaka, Salah amekuwa na msimu wa maisha yake, lakini Liverpool haingekuwa karibu kuwa na nguvu kama ilivyo bila Van Dijk.

Mholanzi huyo alikosa sehemu kubwa ya msimu wa 2020-21 baada ya kuumia.

Sasa kwa vile Virgil van Dijk amerejea kutoka kwenye majeraha yake, mambo yamerejea katika hali yake ya kawaida.

Kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson aliwahi kusema: "Shambulio hushinda mchezo, ulinzi hushinda mataji."

Nukuu hiyo maarufu iko kwenye kesi ya Virgil van Dijk na Liverpool. Tutataja takwimu ili kusisitiza ukweli kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ndiye mchezaji wao muhimu zaidi.

Katika mechi 60 ambazo Virgil van Dijk amecheza Anfield tangu ajiunge nayo Januari 2018, Liverpool wameshinda 52 na sare 8. Hawajawahi kupoteza.

### #1. MANCHESTER CITY - RIYAD MAHREZ


Tofauti na timu nyingine, Manchester City haitegemei kabisa mchezaji yeyote. Ndio maana hawana kigugumizi cha kuangusha wapinzani na kuwazamisha kwenye mabao licha ya kutokuwa na mshambuliaji maalum.

Lakini kama kumekuwa na mchezaji mmoja bora ambaye amewashinda wachezaji wengi wa kiwango cha juu duniani wanaomzunguka msimu huu, ni Riyad Mahrez. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria tayari alikuwa amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji bora kwenye Ligi Kuu kabla ya kampeni inayoendelea.

Hata hivyo, amepanda daraja msimu huu na amegeukia mtu muhimu sana kwa Manchester City. Mahrez amefunga mabao 21 na kutoa asisti saba katika mechi 34 kwenye michuano yote kwa vinara hao wa Ligi Kuu msimu huu.

## Nukuu

"Nchi ambazo zimeingiza timu robo fainali hazizidi tano, lakini kuna watu wanajifanya hawaoni jitihada ambazo zimefanywa na Simba. Mwakani Tanzania tutaingiza tena timu nne kwenye mashindano ya CAF na hizi ni jitihada za Simba," **Mwenyekiti wa Wanachama wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu.**



"Arsenal inapaswa kumsajili [Cristiano] Ronaldo majira haya ya kiangazi. Niko makini sana. Hilo lingetatua tatizo la mshambuliaji wetu na kunisaidia kuondoka kwa [Pierre-Emerick] Aubameyang. Tayari nimemwandalia @Cristiano jezi," **Shabiki maarufu wa Arsenal, Piers Morgan.**



"Nakubaliana na watu wanaosema kuwa hatujafanikiwa Ulaya, hatujashinda ubingwa wa Ulaya huenda wako sahihi, ili kutambulika na kila mtu nje ya Ulaya na duniani ni kutawala soka la Ulaya. Hakuna namna yoyote ya kuwa timu kubwa Ulaya bila kuwa na taji la Ligi ya Mabingwa, kwani hapo ndipo kwenye kipimo kikubwa kwako," **Kocha wa Machester City, Pep Guardiola.**





# CHAMBUA AMULIKA UBORA, UDHAIFU YANGA

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIKA sehemu ya kwanza ya mahojiano haya wiki iliyopita, Sekilojo Chambua, mshambuliaji wa zamani wa Yanga, alitoa tathmini yake kuhusu Kikosi cha Simba na kuzungumzia maisha yake ya kisoka, akiwa na angalizo kwa wachezaji vijana nchini kwamba ajira ya soka ni ya kipindi kifupi.

Leo katika sehemu ya mwisho, Chambua anaangazia ubora na udhaifu wa Kikosi cha Yanga na kukumbusha namna timu hiyo ilivyotekwa jijini Dar es Salaam na kupelekwa Kibaha mkoani Pwani mwaka 994. Endelea kufuatilia mahojiano ya Nipashe na mshambuliaji huyo wa zamani wa Tukuyu Stars:

----

SWALI: Mwaka 1997 uliifunga Simba hapa Dodoma mbele ya aliyekuwa Makamu wa Rais, Dk. Omar Ali Juma. Ulisema goli hilo ni zawadi kwa mwanao Lissa. Yuko wapi kwa sasa na anafanya nini?

CHAMBUA: Ni kweli, hii ilikuwa mechi ya mwisho ya Ligi ya Muungano. Kama unakumbuka zamani kulikuwa na ligi hiyo iliyojumuisha timu tatu za kwanza katika Ligi ya Tanzania Bara na tatu za kwanza kutoka Ligi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, timu hizi sita zilikuwa zinakutanishwa kwenye ligi, tunacheza home and away (nyumbani na ugenini). Hiyo ni mechi ambayo tulikuwa tunacheza pale Uwanja wa Jamhuri Dodoma kati ya Yanga na Simba.

Nililitoa zawadi lile goli kwa mwanangu kwa sababu ndiyo kwanza alikuwa anatimiza mwaka mmoja, maana alizaliwa mwaka 1996. Niliona kuwa goli lile ambalo lilitupa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, liwe zawadi kwake kwa sababu nilifurahi sana.

Nikasema ni zawadi ambayo ninampa binti yangu Lissa. Lissa anafanya kazi TBL kule Dar es Salaam, baada ya kumaliza tu masomo yake Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) aliajiriwa katika kampuni hiyo ya bia.

SWALI: Mgogoro wa Yanga mwaka 1994 uliiathiri timu kwa namna gani?

CHAMBUA: Daaah! Mgogoro kwa kweli uliiathiri timu kwa kiasi kikubwa sana! Ninachokumbuka, kwanza ulisababishwa na mgogoro wa Yanga kwa Yanga. Nikisema hivi ninamaanisha kwamba wakati ule palianzishwa hili suala la Yanga kampuni na kukawa na ule upande unaojiita Yanga asili.

Yanga kampuni ni yale mageuzi ambayo Mzee [Regnald] Mengi alitaka kuyasimamia, kwamba Klabu ya Yanga iendeshwe kama kampuni, lakini pakatokea upande wa pili ambao ukawa unapinga. Miongoni mwa watu waliokuwa wanapinga upande wa Yanga asili ni wale wahindi waliokuwa wanatufadhili kipindi kile, nikimaanisha kwamba ni pamoja na marehemu Abbas Gulamali, marehemu Patwa na wahindi wengine ambao walikuwa wanatufadhili kipindi kile.

Haya makundi ndiyo yalisababisha timu ikatekwa. Timu ilipotekwa, kwa maana tulichukuliwa usiku tukapelekwa Mkoa wa Pwani, Kibaha, tukafichwa huko. Pakatokea mgogoro na fujo nyingi mitaa yote ya Kariakoo hiyo, ilikuwa imezingirwa na polisi kutokana na hayo makundi kutaka kupigana na kujua timu iko wapi.

Bahati nzuri polisi walijitahidi kuzima hayo matatizo ambayo yalikuwa yanaendelea mitaa ya Kariakoo. Na ninakumbuka Waziri wa Mambo ya Ndani kipindi kile, Mzee Mrema, alitumia utaratibu wake wa kutoa siku saba. Akatoa siku saba wahindi wairudishe timu.

Namna gani timu iliathirika? Tulicheza mechi dhidi ya Simba, kukawapo aina fulani ya hujuma kwa baadhi ya wachezaji, tukapoteza mchezo kwa kufungwa magoli 4-1.

Baada ya hapo, uongozi ambao ulikuwa chini ya Katibu Mkuu Mpondela, maarufu Castro, alifukuza wachezaji karibu wote. Ninakumbuka tulibaki wachezaji saba tu, yaani mimi, Kenny Mkapa, marehemu Ally Yusuph Tigana, David Mjanja na baadhi ya wachezaji. Tulibaki saba tu, wengine wote walifukuzwa.

Ililazimika msimu uliofuata kupandisha wachezaji wengi kutoka timu B na kusajili wachezaji wapya. Miongoni mwa wachezaji waliopanda kutoka timu B ni Salehe Romario, Omara Awadh, Silvatus Ibrahim, Mzee Abdallah pamoja na mchezaji ambaye alipata mafanikio sana Ulaya, Mkongo Nonda Shabaan Papii.

Hayo ndiyo mabadiliko au athari zilizoipata timu maana tulilazimika kutengeneza timu mpya kutokana na uongozi kufukuza karibu wachezaji wote na kubakisha saba tu. Ndivyo ninavyokumbuka katika sakata hilo la mwaka 1994.

SWALI: Yanga na Simba zinapokutana kunakuwa na msisimuko wa aina yake. Kipindi chako hali ikuwaje lilipokaribia pambano la watani wa jadi?

CHAMBUA: Ni kweli mechi hizi zinakuwa na mambo mengi sana. Mimi nilipenda kukaa kambini. Maandalizi ya mechi hizi yanakuwa ni makali na ulinzi unakuwa mkali sana kambini, hata kama mko hotelini kunakuwa hakuna kutoka.

Kwa hiyo, nilikuwa sitaki kabisa kukaribisha jambo ambalo kisaikolojia lingeweza kusababisha kunitoa mchezoni, hivyo nilikuwa ninajitahidi sana kutulia, baada ya mazoezi ninapumzika kwa kuangalia televisheni, kufikiri namna gani nitacheza hiyo mechi pamoja na kumwomba Mungu niwe katika hali nzuri.

Mechi za Simba na Yanga zina historia yake ambayo haishi. Kuanzia mwaka 1965, mchezaji anayeshikilia rekodi ya kupiga hat-trick (magoli matatu katika mechi moja) ni mmoja, Mzee King Kibadeni.

Ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kutoka mwaka 1965 mpaka sasa, takwimu zinaonyesha mimi nina magoli saba, wengine wana magoli matano, wengine sita, Kwa hiyo, mimi nina magoli saba niliyoifunga Simba. Ni moja ya rekodi ambayo ninafikiri itakuwa ngumu kufutika.

SWALI: Kwa uzoefu wako wa mechi za kimataifa, hususan ngazi ya klabu, kwa nini mara nyingi timu hata iwe bora ni nadra kushinda ugenini, mfano Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu huu?

CHAMBUA: Ninachoona mimi kuna tatizo katika soka letu la Afrika. Siyo kwamba timu hazishindi ugenini, imeshawahi kutokea, lakini kwa Afrika ni mara chache sana.

Klabu nyingi zimeonekana kutumia zaidi zaidi uwanja wa nyumbani tofauti na wakiwa ugenini. Hii ina tofauti sana na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sababu klabu nyingi zina uwezo wa kushinda hata ugenini.

Tumeona juzi Real Madrid anashinda ugenini dhidi ya Chelsea na Real Madrid huyo huyo kapigwa nyumbani kwake. Tatizo kubwa ninaliona liko kwa waamuzi wetu wanavyochezesha, ninaona kuna mzingira ya timu mwenyeji kubebwa.

Kwa kweli tunatakiwa kuvuka sehemu hii. Kuna visa vingine vingi vinafanyika, ni sababu ambazo mimi ninaona zinachangia timu zetu kushindwa kushinda ugenini pamoja na kwamba kuna kipindi baadhi ya timu zinafanya vizuri ugenini, lakini ni mara chache sana.

**UBORA, UDHAIFU YANGA**

SWALI: Kwa namna Kikosi cha Yanga kilivyo sasa, unafikiri kinahitaji maboresho maeneo yapi ili kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao?

CHAMBUA: Maboresho yanategemea mipango ya mwalimu, lakini mimi ninaona kikosi bado ni kizuri japo kuna wachezaji kadhaa ambao wamekumbwa na majeraha kama Mapinduzi Balama.

Ili Yanga ifanye vizuri msimu ujao, ni lazima aongezwe mshambuliaji ambaye atasaidiana na (Fiston) Mayele kwa sababu mashindano hayo yana mikikimikiki mingi, safu ya ushambuliaji lazima uwe na watu walau wawili wanaolijua lango vizuri.

Mpaka sasa bado Makambo hajadhihirisha anapoingia kwamba anaweza akawa msaidizi mzuri wa Mayele. Kwa sasa kikosi kinaonekana kuwa kizuri, lakini eneo hilo nililolitaja ninafikiri Yanga hawana budi kulitupia jicho.

SWALI: Historia yako ya soka ina milima na mabonde. Lipo tukio la mmoja wa watu wako wa karibu kufariki dunia baada ya kuanguka uwanjani mkoani Mbeya. Uliwezaje kuhimili visa kama hivi?

CHAMBUA: Hii ilikuwa kitambo kidogo wakati huo sijaanza kucheza Ligi Kuu. Kuna rafiki yangu alikuwa anaitwa Frank Mwangomo, alifariki dunia uwanjani, kwenye Uwanja wa Chuo cha Maendeleo Katumba kule Tukuyu wakati huo tulikuwa tunacheza ligi ngazi ya mkoa.

Haikuwa jambo rahisi kwangu kulihimili kwa sababu nilikuwa kijana mdogo sana, kuangukiwa na tukio hilo la kufiwa na mchezaji mwenzangu ambaye nilikuwa ninaishi naye chumba kimoja ilikuwa shida kubwa.

Kuna kipindi nilipata mfadhaiko wa akili, sikuwa katika hali nzuri maana baada ya kufariki dunia, ilibidi nihame, nikiache kile chumba nilichokuwa ninaishi naye kwa sababu nilikuwa sijakomaa kiakili, hivyo nilipata matatizo kifikra.

Ninamshukuru Mungu baada ya hapo nilipata matibabu ya kisaikolojia nikaendelea na shughuli zangu. Kwa kweli ni jambo ambalo kila mmoja wetu kwa kipindi kile tunalikumbuka sana kwa sababu lilikuwa tukio kubwa kwetu kama vijana wa wakati huo.

**JE, WAJUA?**



STRAIKA wa zamani wa Ujerumani, Miroslav Klose, ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi Kombe la Dunia akiwa ametupia mara 16. Lakini pia nchi yake hiyo ndiyo inayoshikilia rekodi ya kucheza nusu fainali nyingi zaidi kwenye michuano hiyo, huku ikitwaa ubingwa huo mara nne; 1954, 1974, 1990 na 2014.





# Mbinu mpya ya kusafirisha wahamiaji haramu yabainika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Uhamiaji mkoani Dodoma limebaini kuwapo kwa mbinu mpya ya kusafirisha wahamiaji haramu kwa kutumia magari madogo badala ya malori kama ilivyokuwa awali.

Aidha, limewakamata raia watano wa Ethiopia ambao wameingia nchini kinyume cha sheria wakiwa kwenye gari ndogo aina ya Toyota Rumioni.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Uhamiaji wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji (ACI), Bahati Mwaifuge, alisema jeshi hilo limegundua mbinu hiyo na kuwataka wanaofanya biashara hiyo kuacha mara moja.

"Pamoja na kubadili mbinu za usafirishaji, Jeshi la Uhamiaji linawaonya wanaofanya biashara ya wahamiaji haramu waache tabia hiyo mara moja,"alisema Mwaifuge.

Kuhusu raia waliokamatwa, alisema pia jeshi hilo linamshikilia Mtanzania Tito Mbwilo (43) ambaye alikuwa akisafirisha raia hao kwa kutumia gari yenye namba za usajili T 991 DXB Toyota Rumioni.

Alisema Mtanzania huyo alikuwa akiwasafirisha wahamiaji hao haramu kwenda Tunduma katika mkoa wa Songwe ili wavuke kwenda Afrika ya Kusini.

Alisema uchunguzi umebaini kuwa Mbwilo ana makazi sehemu mbili ambayo ni Iringa na Tunduma ili iwe rahisi katika kufanikisha biashara yake haramu.

"Jeshi la Uhamiaji liko imara na kazi yake,linapita kila kona kuhakikisha raia wa kigeni wanaingia nchini kwa kufuata taratibu na sheria za nchi," alisema Mwaifuge.

Mwaifuge alisema mtuhumiwa huyo alipokamatwa alijaribu kutoroka, lakini askari wa Uhamiaji walimdhibiti na kumuweka chini ya ulinzi kwa ajili ya kuendelea na taratibu nyingine za kisheria.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano wanapoona kuna raia wanasafirishwa isivyo halali ili Jeshi hilo lichukue hatua kali za kisheria.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifa Omolo, akiwakabidhi watoto wa Kituo cha Rahma, Chang'ombe jijini Dodoma, zawadi ya Sikukuu ya Pasaka, wizara na Wizara ya Fedha Zanzibar, jana walitoa vitu mbalimbali kwenye baadhi ya vituo vya kulea watoto yatima ikiwa ni ishara ya kushirikiana nao kwenye sikukuu hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mamia waliokwama sekondari wafadhiliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MRADI wa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio nje ya Shule (IPOSA), umefadhili wanafunzi zaidi ya 400 wa Halmashauri ya Mji Kondoa kupitia elimu ya watu wazima kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 14 walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Gift Kyando, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya siku 13 kwa wawezeshaji waliopata mafunzo kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu wazima wakishirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ambapo mpango huo unafadhiliwa na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF). Mpango huo utatekelezwa katika vituo vya shule za Msingi Kolo, King'ang'a, Maji ya Shamba, Modeli na Chandimo ambapo masomo ya useremala, uashi, ushonaji, usindikaji wa vyakula na utengenezaji wa batiki yatatolewa kwa miezi mitatu. Kyando alisema wanafunzi hao watakapohitimu wataonyesha matokeo chanya kwa vijana ili kuitendea haki rasilimali fedha iliyogharamikia mafunzo hayo.

Alisisitiza maofisa elimu kata kusimamia vyema na kutoa mrejesho katika kila hatua inayoendelea kulingana na mafunzo yaliyotolewa.

"Siku 13 mlizokaa ziende kuleta matokeo chanya,sio mnaenda kuleta mzaha, niwasihi sana kaka na dada zangu muende mkawe taa njema. Maofisa elimu kata simamieni vizuri ili aliyepata elimu alete tija kama haleti tija tuambieni ukweli kuwa tuliomchagua tulikosea," alisema. Alieleza kuwa wanataka kuona shule za msingi na sekondari zitakwenda kutumia sabuni watakazo kuwa wanazalisha baada ya kupata mafunzo hayo.

Awali, akisoma risala kwa mgeni rasmi Mwalimu Emile Abel, alisema wamejifunza maarifa na ujuzi mbalimbali ikiwamo usindikaji wa vyakula na utengenezaji wa batiki.

Alisema pamoja na kupata elimu hiyo wameiomba Serikali kuwaletea mapema vifaa vya kufundishia na kujifunzia kulingana na idadi ya wanafunzi ili wanafunzi wapate ujuzi kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kupatiwa vyumba maalum kwa ajili ya kuhifadhia kemikali.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Irene Mosha, alisema wapo tayari kutoa mikopo ya vifaa ili kuendeleza mpango madhubuti wa serikali utakaosaidia kuipaisha Kondoa katika maendeleo ya viwanda.

"Ofisi ya Halmashauri tupo tayari kutoa mikopo ya vifaa kwa ajili ya kuendeleza hili zoezi na Kondoa tuliyonayo sasa inakwenda kubadilika baada ya muda fulani," alisema.

# Karakana za ufundi za wenye ulemavu zaombewa ruzuku

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kutoa ruzuku kwa karakana za ufundi za watu wenye ulemavu, ili kusaidia kuzalisha vifaa visaidizi kwa ajili ya watu hao badala ya kuagiza nje ya nchi.

Fundi Mkuu wa Karakana ya Walemavu Mkoa wa Dodoma (KAWADO), Mwita Marwa, alitoa ombi hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema ruzuku hiyo ikitolewa kwenye vyuo vya ufundi vya watu wenye ulemavu, itasaidia kuzalisha vifaa mbalimbali visaidizi vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu na kuondokana na gharama kubwa ya kuagiza nje ya nchi.

Aidha, alisema vifaa hivyo vitasaidia shughuli zao za kila siku za kiufundi ili kujikimu kimaisha kutokana na walio wengi kujikuta wapo majumbani na mitaani huku wakiwa wana ujuzi.

"Ofisi ya Waziri Mkuu hivi sasa imefungua vyuo vyake vya serikali kwa ajili ya watu wenye ulemavu, ili waweze kujiunga na kujifunza elimu ya ufundi ambayo itawawezesha kuondokana na hali ya kutegemea utegemezi," alisema.

Alisema fursa hiyo iliyofunguliwa na serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu itawafanya kujiinua kiuchumi zaidi kutokana na elimu inayotolewa ya mafunzo ya ufundi bure.

"Mimi pamoja na kuwa nina Karakana hii ya ufundi ambapo pia ni mlemavu wa viungo,ninawaomba walemavu wezangu kuchangamkia hiyo fursa ya kujiunga kwenye vyuo vya ufundi ikiwemo vya serikali na watu binafsi ili waweze kujikwamua kimapato"alisema.

Marwa alitoa rai kwa wazazi na walezi wasiwaweke vijana majumbani, bali wawaelekeze kwenye vyuo mbalimbali vya ufundi kulingana na ulemavu walionao ili wapatiwe ujuzi.

"Bado kuna ukatili wa kuwakosesha haki ya kimsingi watu wenye ulemavu ambao bado wanafichwa majumbani wakati fursa ya kuwaendeleza kwenye vyuo vya ufundi ipo,"alisema.





## Spika Tulia ahimiza wananchi kushiriki kwenye maendeleo

**Na Nerbert Msoka,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka wananchi kuenelea kuiunga mkono Serikali kwa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo katika maeneo yao badala ya kuiachia serikali kila kitu.

Aliyasma hayo juzi katika Mji wa Makongolosi wilayani Chunya aliposhiriki kwenye hafla maalumu ya kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza mwaka mmoja madarakano ilitoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT) wa wilaya hiyo.

Aidha, hafla hiyo ilikuwa na lengo la kumpongeza Dk. Tulia kwa kuchaguliwa kuwa Spika baada ya aliyekuwa anashikilia nafasi hiyo, Job Ndugai, kujiuzulu wadhifa huo miezi michache iliyopita.

Alisema Serikali inafanya juhudi ya kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo ya sekta ya elimu, afya, barabara, viwanja vya ndege na miundombinu mingine na hivyo akawataka wananchi nao kushiriki kuijenga ile ambayo wanaweza.

"Serikali pekee haiwezi kuyatekeleza yote haya kwa wakati, hivyo niwaombe ndugu zangu nanyi mshiriki kwenye ujenzi wa baadhi ya miundombinu hii hasa ya elimu na afya ambayo inawagusa moja kwa moja," alisema Dk. Tulia.

Alisema baadhi ya miradi ya maendeleo huibuliwa na wananchi na serikali ikiona juhudi za wananchi ndipo huingia na kuwaunga mkono wananchi hao kwa kutoa raslimali mbalimbali.

Dk. Tulia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa rais Samia madarakani miradi mingi ya maendeleo nchini imetekelezwa na kwamba wananchi wanatakiwa waendelee kumuombea kiongozi huyo ili alete maendeeleo zaidi.

# Waziri awapa kibano maofisa wa TAZARA

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amewakalia kooni maofisa wa Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kwenye kiwanda cha kuzalisha kokoto cha Kongolo Mswiswi kilichopo wilayani Mbarali na kubaini madudu kadhaa.

Mwakibete amebaini mtambo wa kuchorongea mawe uliononuliwa na maofisa hao ukiwa haufanyi kazi kutokana na sababu ambazo hazieleweki na baadhi ya mitambo ikiwa imeegeshwa kwenye karakana ya kiwanda hicho bila sababu.

Naibu Waziri alifanya ziara hiyo juzi baada ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu kudai kuwa baadhi ya mitambo iliyonunuliwa na shirika hilo kwa fedha nyingi haifanyi kazi kutokana na kuwa mibovu ambapo alisema aliamua kwenda kujiridhisha.

Alipowahoji maofisa hao kuhusiana na mtambo huo walieleza ni mzima na unafanya kazi na ndipo alipoamua kwenda kuukagua ulipoegeshwa na ndipo alipoanza kuwa na wasiwasi baada ya kuona eneo ulipo unaashiria kuwa umekaa kwa muda mrefu.

Alimtaka mtaalamu anayeendesha mtambo huo auwashe ili athibitishe kuwa ni mzima ama sio mzima, lakini ilishindikana baada ya mtaalamu huyo kumweleza kwamba hauna mafuta, hivyo hauwezi kuwaka.

"Mimi naamini mtambo huu sio mzima kama ambavyo Kamati ya Bunge ililalamika, nilitaka uwake ili nijiridhishe lakini nashindwa kuthibitisha kama ni mzima ama sio mzima kwa sababu haujawaka, sasa nataka nitakapopita tena hapa nikute mtambo unafanya kazi," alisema Mwakibete.

Aliutaka uongozi wa TAZARA makao makuu ambao ndio wenye jukumu la kuhakikisha kiwanda hicho cha Kongolo Mswiswi kinapata mafuta kuidhinisha mafuta hayo kila yanapohitajika ili kazi zinazofanyika hapo kutokwama.

Meneja wa mgodi wa kuzalisha kokoto wa kiwanda hicho, Idd Abdallah, alisema mtambo huo pamoja na mingine miwili waliinunua kwa zaidi ya Sh. bilioni 2.005 lakini huo wa kuchoronga miamba ulikuja tofauti na waliokuwa wanauhitaji.

Alisema pamoja na kwamba una tofauti lakini ufanisi wake ni mzuri kuliko waliokuwa wanautumia zamani ambao ulikuwa unazalisha tani 600 za kokoto kwa siku lakini mpya walionunua unazalisha zaidi ya tani 1000.

Alisema baadhi ya kokoto wanazozalisha zinatumiwa na shirika kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli nzima kuanzia mkoani Dar es Salaam mpaka Kapirimposhi Zambia ambayo ina urefu wa zaidi ya Kilomita 1800 na zingine wanaziuza kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

"Mafuta tunayotumia hapa tunaletewa kutoka Makao Makuu lakini mpaka sasa hatujaletewa na ndiyo maana unauona mtambo huu umeegeshwa hapo lakini tukiletewa mafuta tutaendelea na kazi," alisema Abdalla.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA, Christopher Shiganza, alisema kwa sasa shughuli za shirika hilo zimepungua kutokana na daraja la reli kuharibika katika eneo la Chambeshi nchini Zambia.

Alisema hata vyanzo vya mapato vimepungua kwa maelezo kuwa wanategemea zaidi kusafirisha shaba inayozalishwa katika eneo la Copper Belt nchini Zambia.

Licha ya ubovu wa mtambo huo, pia naibu waziri alibaini kuwa hata uzalishaji wa mataluma ya reli unaotakiwa kufanyika katika kiwanda hicho umesimama kwa muda usiojulikana huku maofisa wa TAZARA wakidai kuwa wameishiwa saruji.

Vilevile alibaini kuwa hakuna uhusiano mzuri kati ya kiwanda hicho na wananchi wa vijiji vinavyouzunguka ambapo Mwenyekiti wa Kijiji, Ofisa mtendaji na Diwani walidai kuwa kiwanda hicho hakiwasaidii kwenye shughuli za maendeleo.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wa pili kulia) akisikiliza maelezo ya utengenezaji wa mataluma kutoka kwa maofisa wa Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) alipofanya ziara kwenye Kiwanda cha Shirika hilo cha Kongolo Mswiswi katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Sababu kushuka kitaaluma shule za CCM zabainishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUMUIYA ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) imesema moja ya mambo yaliyosababisha shule inazozimiliki kushuka kitaaluma na baadhi yake kuwa katika hatari ya kufungwa, ni ubadhirifu uliofanywa na baadhi ya viongozi wasiokuwa waaminifu.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Gilbert Kalima, alibainisha sababu hizo jijini Mbeya alipokuwa anatangaza matokeo ya mtihani maalumu wa kuwapima wanafunzi wa kidato cha sita wanaosoma kwenye shule 14 za Jumuiya hiyo nchini.

Alisema baadhi ya wasimamizi wa shule hizo waliokuwa wameaminiwa na Jumuiya hiyo ndio walifanya ubadhirifu huo ambao umezifanya shule hizo kuwa na hali mbaya na kwamba baadhi yake zimekimbiwa na wanafunzi.

Alizitaja sababu zingine kuwa ni serikali kuboresha shule zake za kata kwa kuhakikisha zinakuwa na miundombinu bora pamoja na vifaa vya kusomea hali ambayo imewafanya wazazi wengi kuanza kuziamini na kuwapeleka watoto wao huko.

Vilevile, alisema sera ya 'Elimu Bila Malipo' inayotekelezwa na serikali pia ni sababu mojawapo iliyosababisha shule za jumuiya hiyo kushuka kitaaluma kwa maelezo kuwa wazazi wengi wanawapeleka watoto wao kwenye shule za serikali badala ya shule binafsi zikiwamo za jumuiya hiyo.

"Lakini sasa hivi tupo kwenye mikakati maalumu ya kuziboresha shule zetu zote ili sasa zirejee katika hali yake ya awali, moja ya mikakati ni kuimarisha usimamizi, kuboresha miundombinu ya shule na kuanzisha mitihani ya mara kwa mara kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi wetu," alisema Kalima.

Akitangaza matokeo ya mtihani huo maalumu, Kalima alisema ulishirikisha wanafunzi 1,202 ambao kati yao wanafunzi 984 ni watahiniwa wa shule na wengine 218 ni watahiniwa wa kujitegemea, na kwamba ambao hawakufanya mtihani huo walikuwa 37.


Alisema kwenye mtihani huo wanafunzi wamefanya vizuri kwa maelezo kuwa waliofaulu kwa kupata daraja la kwanza walikuwa 148, daraja la pili 394, daraja la tatu 369, la nne 33 na kwamba hakuna mwanafunzi aliyepata daraja sifuri.

Alizitaja shule tano vinara kuwa ni Wari Sekondari ya mkoani Kilimanjaro, Shule ya Sekondari Mombo (Tanga), Shule ya Sekondari Ivumwe iliyopo mkoani Mbeya, Shule ya Sekondari Mwembetogwa (Iringa) na Shule ya Sekondari Sangu (Mbeya).

"Shule ambazo ufaulu wake ni hafifu ni Shule ya Sekondari Kasulu na Shule ya Sekondari Ujiji zote za mkoani Kilimanjaro na Shule ya Sekondari Mwanga iliyopo mkoani Kilimanjaro, hizi tumetoa maelekezo maalumu kwa walimu na bodi za shule ili waongeze ufaulu," alisema Kalima.

Alisema jumuiya hiyo haina mpango wa kuziuza wala kuzibadilisha matumizi shule hizo kama ilivyokuwa inazungumzwa mitaani na kwamba uvumi huo ulisababisha baadhi ya wazazi kuwa na wasiwasi na kuamua kuwahamishia watoto wao kwenye baadhi ya shule.






Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi wa pili (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 20 mshindi wa kwanza katika Mashindano ya 22 ya Kuhifadhi Qur'aan Afrika, Thiame Bouna, kutoka Congo Brazaville, yaliyofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya BPZ, Dk. Muksin Masoud, na wapili kulia ni Rais wa Taasisi ya Al- Hikma, Abdulqadir Al-Hadar waandaaji wa mashindano hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu: Pasaka yagubikwa uchungu wa vita

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Agostino Shao, amesema kuwa furaha ya Sikukuu ya Pasaka imegubikwa na uchungu wa vita vinavyoendelea nchi nyingi duniani hasa vya Russia na Ukraine ambavyo vimeathiri maisha ya watu wengi.

Aliyasema hayo jana katika ibada maalum ya Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika katika kanisa hilo, Shangani mjini hapa.

Alisema mfumuko wa bei za bidhaa muhimu kama mafuta umeathiri nchi nyingi ikiwamo Tanzania na kwa sababu ya ugumu wa maisha watu wengi wameshindwa kusherehekea shangwe za Kristo kufufuka na jamaa zao.

"Tunaomba serikali zetu mbili zitafute njia ya kufidia gharama za mafuta kwa kupunguza tozo za mafuta na kuweka bei inayoeleweka," alisema.

Alisema bei elekezi zilizowekwa zinamuumiza mnunuzi na kumfaidisha muuzaji na alishauri kuwekwa kwa bei ya wastani baada ya kujifunza gharama za usafirishaji na nyinginezo.

"Ndugu zangu tutakuwa tumejidanganya kama aleluya kuu tunayoimba leo na siku zote haitaleta furaha na mwanga kwa mataifa na kujenga matumaini kwa wanaoteseka magerezani na rumande kwa kukosa haki."

Alisema kuwa Kristo aliyefufuka hawezi kukemea hayo kwa mdomo wake, mikono yake na miguu yake bali kuwa na upendo miongoni mwao kwa wale wanaoteseka.

"Naomba sote tuwe alama ya matumaini na furaha kwa wote wanaoteseka na kamwe tusikubali kusherehekea siku ya leo wenyewe, tujaribu sana kuwapelekea furaha za Kristo Mfufuko wale wanaomuheshimu Kristo kwa mateso," alisema.

Alipongeza juhudi za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, za kutoa agizo kwamba kesi za ubakaji, ulawiti na ubaradhuli zisiwe na dhamana za ziwe ni kesi za jinai na mahakama kuu pekee ndiyo zishughulikie kesi hizo.

Alisema kutokana na agizo hilo kumekuwa na unafuu mkubwa wa kesi hizo nyingi za aina hiyo hazichukui tena muda mrefu, lakini jambo la kushangaza bado muhali unatesa jamii kwa sababu ya kumhurumia mtuhumiwa kuliko aliyeumizwa.

Alisema ni lazima kushughulikia kero za jamii, kuna tatizo la usafirishaji haramu wa binadamu na baadhi ya wahusika wakubwa wanafahamika, lakini kwa sababu ya kulinda maovu na tatizo la muhali wanakaa kimya.

Akizungumzia kuhusu mashine za kielektroniki, alisema bado baadhi ya wafanyabiashara wakubwa hawana mashine hizo za utoaji wa risiti na bidhaa nyingi zinazouzwa hazijalipiwa ushuru na kuziomba taasisi husika kulifuatilia hilo kwa sababu kila raia akilipa kodi maendeleo yataimarika.

# Maslahi ya madaktari, wahudumu afya kutekelezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ahadi ya serikali ya kuimarisha maslahi ya madaktari, wahudumu na wafanyakazi wa kada ya afya bado ipo na itatekelezwa mapema iwezekanavyo.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa kongamano la pili la madaktari na wahudumu wa afya, lililofanyika, mjini hapa.

Alisema kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na madaktari, wahudumu na wafanyakazi wa kada ya afya, serikali imeweka mazingatio maalum ya kuimarisha stahiki zao ili kuimarisha utendaji wa kazi.

Alisema baada ya kupitia upya maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya afya Zanzibar imebainika kuwa hayaendani na 'scheme of service' na kubainisha miongoni mwa kasoro iliyopo ni ya wafanyakazi wa muda mrefu kupata maslahi duni na kwamba hatua ya serikali ya kutoa maslahi itaambatana na mfumo huo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeweka kipaumbele kuimarisha sekta ya afya, ikianzia na uimarishaji wa miundombinu kwa kuhakikisha kila wilaya inakuwa na hospitali ya kisasa ili kuwaondolea usumbufu wananchi kufuata matibabu nje za wilaya zao wanazoishi.

Alisema serikali inaendelea na kazi ya kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma pamoja na kugharamia upatikanaji wa huduma za afya kupitia mfumo wa Bima ya Afya. "Dhamira ya serikali ni kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya kila mwaka ili kuwa na uwezo wa kununua dawa na vifaa tiba, kusomesha madaktari na wauguzi pamoja na kuongeza idadi ya madaktari bingwa na wafanyakazi, sambamba kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa matibabu," alisema.

Alisema kuwa ushirikiano unaoendelea kati ya Taasisi ya Jamiiyatul Akhalaqul Islamia (JAI) na serikali zote mbili, unakwenda sambamba na malengo ya Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya nchini.

Alisema amevutiwa na kaulimbiu ya kongamano hilo isemayo 'Malipo ya wema ni wema' na kubainisha mafundisho na mazingatio makubwa yaliyomo ndani yake kwa madaktari na wauguzi, kuwa wana dhima ya kutoa huduma muhimu za afya katika mazingira mbalimbali.

Naye, Waziri wa Afya Ahmeid Nassor Mazrui, alisema wizara yake imekuwa ikitupiwa lawama nyingi dhidi ya wauguzi wake kutokana na dosari mbalimbali wanazozionyesha katika utendaji wao, ikiwamo utoaji wa kauli mbaya kwa wagonjwa.

Alisema kuwa ipo haja ya kupandishwa daraja utoaji wa huduma kwa wagonjwa ili kuwajenga imani.

Alisema wakati serikali ikijiandaa kuingia katika mpango wa utoaji wa huduma ya Bima ya Afya, kuna umuhimu kwa watendaji wa wizara hiyo, ikiwamo madaktari na wauguzi kutoa huduma bora.

Akiwasilisha risala ya Taasisi ya Jamiiyatul AkhlaqulIslamia, Naibu Katibu Mkuu wa taasisi hiyo, Khalid Rajab, alisema lengo la kongamano hilo ni kuwaita madaktari na wauguzi pamoja na wafanyakazi wa kada ya afya, kuangalia namna bora ya kufanyakazi zao kwa misingi ya dini.

# Ujerumani yatoa bil. 1.7/- upatikanaji majisafi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Ujerumani imetoa Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kufanya upembuzi yakinifu utafiti wa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Zanzibar kwa lengo la kujua kiini cha tatizo la uhaba wa huduma hiyo.

Hatua hiyo imekuja miezi miwili tangu Ujerumani kutangaza rasmi kurudisha uhusiano wake na Zanzibar na makubaliano hayo yalifikiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na balozi wa Ujerumani nchini Regine Hess, Ikulu Zanzibar.

Utiaji saini wa makubaliano hayo umefanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka Majisafi na Salama (ZAWA), Dk. Salha Mohamed Kassim na kushuhudiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Maliki Juma Akili na kwa upande wa Ujerumani iliwakilishwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Misaada la Kimataifa la Ufundi la Ujerumani (KFW), Andrea Hoeltke.

Mkurugenzi wa ZAWA, Dk. Salha, alisema msaada huo umelenga kufanya kazi za utafiti za upatikanaji majisafi na salama Zanzibar katika kazi za kitaalamu zaidi.

Alisema mradi huo utafanya kazi za utafiti kujua kiini cha tatizo la majisafi na salama Zanzibar pamoja na kujua vyanzo vya maji vilivyopo. "Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la kimataifa la misaada ya kiufundi (KFW) wamekubali kutoa fedha Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya kufanya kazi za utafiti juu ya upatikanaji wa huduma za majisafi na salama Zanzibar na pia wanataka kujua idadi ya watu wanaopata huduma hiyo," alisema.

Naye Naibu Mkurugenzi wa ufundi wa KFW, Andrea Hoeltke, alisema wamejipanga kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma ya majisafi na salama bila ya matatizo na katika hatua za awali watafanya utafiti kujua kiini cha tatizo hilo.

Alisema makubaliano ya kazi za utafiti huo yamekuja kutokana na Serikali ya Ujerumani kurudisha uhusiano wake na Zanzibar na kuahidi kusaidia harakati za maendeleo na uchumi. "Ujerumani tumetangaza kurudisha uhusiano wetu na Zanzibar ambapo tumeahidi kusaidia katika miradi mbalimbali ikiwamo kulipatia ufumbuzi tatizo la majisafi na salama kwa wananchi wa Zanzibar na tutafanya utafiti wa kina kujua kiini chake," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya, alipongeza nia ya Ujerumani inayotokana na ahadi yake ya kuisaidia Zanzibar katika upatikanaji wa huduma za majisafi na salama kwa kufanya utafiti.

Dk. Mkuya alikiri kuwa licha ya juhudi za serikali kulipatia ufumbuzi tatizo hilo kwa utekeleza miradi mbalimbali ya maji, bado wananchi wanahangaika kuitafuta huduma hiyo wakiwamo wanawake.

"Nimefurahishwa na nia ya dhati ya Ujerumani kutekeleza ahadi zake za kufanya utafiti upatikanaji wa huduma za majisafi na salama kwa wananchi wa Zanzibar," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Juma Maliki Akili, alisema Ujerumani ni miongoni mwa nchi za mwanzo baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari mwaka 1964 kusaidia kisiwa hicho misaada mbalimbali ikiwamo ujenzi wa nyumba za kwanza za maendeleo ziliopo Kilimani, Unguja.

"Ujerumani ni rafiki wa kweli wa Zanzibar ambapo tumefurahishwa na juhudi zake za kuamua kuisaidia tena na safari hii katika eneo la utafiti wa upatikanaji wa huduma za majisafi na salama Zanzibar," alisema.

# CAG: Uhai wa Ngorongoro shakani

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ametilia shaka uendelevu wa urithi wa nchi hasa katika kurejesha maeneo ya utalii, ikiwamo Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Amesema mamlaka hiyo inakabiliwa na tishio linalotokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu ndani ya eneo la hifadhi kinyume cha sheria.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowalishwa bungeni jijini hapa Jumanne iliyopita, CAG Charles Kichere anasema kuwa kwenye ripoti ya mwaka 2019/20 alieleza wasiwasi wake juu ya dosari zinazotishia uendelevu wa urithi wa nchi hasa katika kurejesha maeneo ya utalii.

CAG anafafanua kuwa katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) alionyesha tishio linalotokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu ndani ya eneo la hifadhi kinyume cha vifungu vya 6, 23, 24 na 35 vya Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284.

Anasema tishio hilo ni pamoja na miundombinu ya kudumu na matumizi ya pikipiki ndani ya eneo la hifadhi linalosababisha ugumu kwa askari wa wanyamapori kutofautisha majangili na watumiaji wa kawaida.

CAG anasema masuala mengine hatarishi ni kutofuata matumizi halali ya eneo, ujangili na kuongezeka kwa uvamizi na kuziba njia za kupita wanyamapori wanapohama (shoroba) na kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori.

"Shughuli hizi zote zinaingilia mfumo wa ikolojia ya eneo. Matokeo yake, kumekuwa na matatizo katika kutekeleza programu za uhifadhi kutokana na ongezeko kubwa la watu na mifugo na uharibifu mkubwa wa mazingira unaohatarisha uhifadhi na kuwapo kwa wanyamapori.

"Nilipendekeza kuwa serikali ichukue uamuzi wa kusitisha mara moja shughuli zinazohatarisha mfumo wa ikolojia ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; kuimarisha mchakato wa kurejesha mfumo wa ikolojia na kudhibiti idadi ya watu na mifugo ili kuwa na idadi inayofaa ambayo itahakikisha uendelevu wa shughuli za uhifadhi katika eneo hilo," anakumbusha.

CAG anasema katika ukaguzi wake mpya wa mwaka 2020/21, ameona maendeleo madogo katika utekelezaji wa mapendekezo yake kwa vile upungufu uliobainika bado unaendelea kubakia.

Anasema mapitio ya Ripoti ya Tathmini ya Mwaka wa 2021 kuhusu mafanikio ya Mpangomkakati wa NCAA wa mwaka 2017 hadi 2021 yalibaini kuwa mpango huo haukutekelezwa kwa sababu ya kugomewa na wakazi wa eneo hilo la Ngorongoro.

"Kwa mfano, katika ufugaji, mkakati ulilenga kuweka mipaka inayoonekana ya malisho ya mifugo katika maeneo yaliyokubaliwa lakini wakazi waligoma na hivyo kuwapo kwa shinikizo la malisho kati ya mifugo na wanyamapori.

"Aidha, imebainika kuwa vijiji vyenye migogoro ya mipaka vimeongezeka kutoka vinne mwaka 2017 hadi 25 mwaka 2020. Matukio ya uvamizi wa maeneo yaliyozuiwa pia yameongezeka kwani mifugo ya wakazi ilichukuliwa katika maeneo ya Embakai na Olmoti Craters pamoja na Msitu wa Nyanda za Juu Kaskazini ambao ni chanzo cha maji cha Karatu, Manyara, Monduli na maeneo yote ya Ngorongoro.

"Mbali na kasoro zilizotajwa, niliendelea kubaini masuala ambayo bado yanaiweka Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro hatarini kwa uendelevu wake. Kwa mfano, pamoja na mambo mengine, kulikuwa na mauaji ya pundamilia wanane (8) kwa kutumia mikuki katika Ukanda wa Enduleni ndani ya hifadhi.

"Ni maoni yangu kuwa iwapo uamuzi wa kimkakati hautachukuliwa katika kupitia upya kazi za NCAA, kuna uwezekano wa uendelevu wa hifadhi hiyo kuwa hatarini," anatahadharisha.

CAG anarudia mapendekezo yake ya awali kuwa serikali itafute njia mbadala za maendeleo ya watu katika maeneo yanayopakana au yanayoingiliana na maeneo ya utalii ili kuimarisha programu za uhifadhi kwa jamii ndani na nje ya maeneo ya utalii.

Pili; CAG anapendekeza serikali ianze mapitio ya muundo wa matumizi bora ya ardhi ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kwa nia ya kupunguza shughuli za maendeleo ya binadamu katika eneo hilo na kuimarisha programu za uhifadhi.

**MUUNDO USIO WAZI**

CAG pia anasema amebaini muundo usio wazi wa utawala baada ya mabadiliko ya NCAA kuwa taasisi ya kijeshi, akiwa na angalizo kwamba kunasababisha vihatarishi vilivyoripotiwa kuathiri shughuli za mamlaka hiyo.

Anafafanua kuwa Sheria ya Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Sura ya 284 (marekebisho ya mwaka 2002) inaelekeza kuwa kazi ya uangalizi wa NCAA iko chini ya bodi ya wakurugenzi ya hifadhi ya eneo hilo.

Hata hivyo, CAG anasema baada ya muda wa bodi ya wakurugenzi ya mamlaka kuisha mnamo Novemba 2020, na baada ya NCAA kubadilishwa kuwa taasisi ya kijeshi, alibaini kuwa muundo wa usimamizi wa mamlaka bado haujafafanuliwa na haupo wazi.



Wasamaria wema mjini Iringa wakisaidia kutenganisha bodaboda zilizogongana jana eneo la Eso Miyonboni, mjini Iringa wakati mmoja akiingia barabara kuu ya Iringa-Dodoma bila tahadhari na kugongana na nyingine iliyokuwa ikikimbiza pilau la Pasaka kwa mteja. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Ujenzi vituo neema kwa wafanyabiashara

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema vituo vya wajasiriamali vinavyo jengwa kote visiwani Zanzibar vitawasaidia kufanya biashara zao kwa uhakika.

Aliyasema hayo wakati akikagua ujenzi wa vituo hivyo, Tumbe katika Wilaya ya Micheweni na Kifumbikai wilayani Wete.

Makamu wa pili huyo alisema , kabla ya kuanza kwa ujenzi huo wananchi walikuwa wakiomba kupata mahali salama pa kufanyia shughuli zao za kazi na biashara ambapo sasa wataweza kupata mahala penye ubora wa kufanyia shughuli hizo na kukuza vipato vyao.

"Namuagiza mkandarasi ahakikishe anamaliza kazi haraka iwezekanavyo kama ilivyo katika makubaliano bila ya kukwama ili wananchi waweze kuvitumia kama ilivyo kusudiwa kujenga vituo hivyo," alisema.

Katika hatua nyingine Makamu huyo wa pili wa rais aliuagiza uongozi wa wizara ya Elimu kusimamia ujenzi wa madarasa katika eneo lolote la ujenzi ili kuhakikisha kunakuwepo utaratibu na vigezo maalum vya uwiano wa ukubwa wa madarasa

Alisema ni vyema ujenzi wa madarasa haya mapya ukaenda sambamba na kiwango kinachokubalika na hilo litaweza kufanikiwa endapo wizara itajitoa kwa kusimamia kila mahala kwenye ujenzi wa madarasa hayo mapya visiwani Zanzibar.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mussa, alisema kukamilika kwa madarasa hayo kutaondoa changamoto ya ufinyu wa madarasa unaisumbua Zanzibar kwa sasa.

Waziri Lela alisema wizara itasimamia kuhakikisha kuwa madarasa yanapata vifaa vyote muhimu ikiwamo taa ili yawe katika hadhi inayohitajika na wanafunzi wasome katika madarasa mazuri.

Kwa upande wake Komodoo Azana Msingira kutoka kampuni ya KMKM Construction Limited amemhakikishia Makamu wa pili wa Rais kuwa pamoja na changamoto za usafirishaji vifaa visiwani miradi hiyo itamalizika kwa wakati .

# Sababu ujenzi shule sekondari kusuasua

**Na Said Hamdani,** LINDI

USHIRIKI mdogo wa wananchi kujitolea nguvu kazi, kutokuwepo miundombinu ya barabara na itikadi za kisiasa ni miongoni mwa sababu zinazotajwa kusuasua ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Kivinje, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi.

Shule hiyo mpya ambayo serikali imeipatia Sh. milioni 70 inajengwa katika Kitongoji cha Mayungi yungi,Kijiji cha Kisangi.

Madai hayo yametolewa na baadhi ya wakazi wa eneo husika, wakiwamo viongozi mbalimbali wa Serikali ya Kijiji hicho na msimamizi wa ujenzi wa shule hiyo, Laurent Suka walipokuwa wanazungumza na waandishi wa habari waliotembelea kuona shughuli za maendeleo zinazofanywa na jamii.

Suka, ambaye pia ni Mkuu wa Sekondari ya Kivinje, alisema wamepokea fedha hizo kutoka Serikalini, kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa, na kwamba kazi ya ujenzi imeshaanza.

Alisema licha ya kazi ya ujenzi kuanza, inakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ushiriki mdogo wa jamii kujitolea nguvu kazi, ambayo inachangia kasi ndogo ya ujenzi, huku akiwaomba wananchi kujitokeza kushiriki ujenzi wake kuwawezesha watoto kupata mahali rafiki pa kusomea.

Alitaja changamoto nyingine ni kutokuwapo kwa barabara inayoweza kutumiwa na magari ya kubeba vifaa kama saruji, mawe, mchanga, nondo na kokoto kufika eneo husika.

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:



Rais Uhuru Kenyatta akiwa na kiongozi wa ODM, Raila Odinga katika moja ya mikutano yao. **PICHA:MTANDAO**

# Uhuru kuongoza Azimio la Umoja

- Kushughulikia nidhamu ya wabunge
- Odinga naye, apitia vikwazo kuifikia Ikulu

**Nairobi,** KENYA

AGOSTI, mwaka huu Kenya utafanyika uchaguzi mkuu, huku muungano wa vyama 26 uitwao Azimio la Umoja-One Kenya, ukimteua Raila Odinga kuwania nafasi ya urais.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa mwishoni mwa wiki, kwenye gazeti la serikali, ni kwamba Rais Uhuru Kenyatta atakuwa Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya.

Odinga atakuwa kiongozi wa muungano huo, Kalonzo Musyoka akiwa kinara wa Wiper, kiongozi wa KANU akiwa Gideon Moi, huku Gavana wa Mombasa Hassan Joho, mbunge wa Murang'a Sabina Chege na mbunge wa Taita Taveta, Naomi Shaban wakiwa wajumbe wa baraza hilo.

Wajumbe wengine watakuwa ni viongozi wa NARC Kenya, Martha Karua, Gavana wa Kitui Charity Ngilu, Abdi Noor Omar Farah na kiongozi wa chama cha Democratic Action Party - Kenya (DAP-K) Wafula Wamunyinyi.

Mbunge wa Suna Mashariki Junet Mohamed atakuwa Katibu Mkuu wa baraza hilo.

Pia, katika muungano ni kwamba wajumbe wa baraza hilo watakutana angalau mara moja baada ya miezi mitatu.

Mwenyekiti ambaye ni Rais Kenyatta ameyabeba mamlaka ya kuitisha kikao hicho cha baraza hilo wakati wowote.

"Wajumbe wa Baraza Kuu watakutana angalau mara moja baada ya miezi mitatu au wakati wowote kulingana na maelekezo ya mwenyekiti," inasema Katiba hiyo.

Baada ya Uchaguzi Mkuu, wabunge wa vyama 26 vilivyo ndani ya muungano huo, wataunda vuguvugu ambalo pia litajumuisha wabunge maalumu na wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Jukumu la vuguvugu hilo litakuwa kutetea sera za serikali ya muungano bungeni, ingawa Rais Kenyatta atakuwa na sauti kuu katika uteuzi wa kiongozi wa vuguvugu hilo la wabunge.

> Ikimaanisha kuwa upande wa Rais Kenyatta huenda ukawa na wabunge wengi zaidi ikilinganishwa na vyama vingine ndani ya muungano, hivyo kuwa na usemi mkubwa.

Na iwapo kutakuwa na jambo lenye utata ambalo litagawanya wajumbe wa Baraza Kuu la Azimio, Rais Kenyatta, ambaye wakati huo atakuwa Rais Mstaafu wakati huo, atapiga kura ya kuamua.

Rais Kenyatta pia atakuwa ndiye msemaji mkuu katika uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Nidhamu, ambayo itapambana na wabunge wa Azimio wanaokiuka maadili kwa kuendeleza ajenda za mrengo wa upinzani.

### NIDHAMU YA WABUNGE WAKOROFI CHAMANI

Baraza Kuu ambalo mwenyekiti wake ni Rais Kenyatta pia linaweza kutambua wabunge wakorofi na kuagiza kamati ya nidhamu kuwashughulikia.

Kamati ya nidhamu, imepewa mamlaka ya kutoza faini, kutimua chamani au kuondoa mbunge kutoka kwenye kamati za Bunge.

Katiba ya Azimio imempa Rais Kenyatta na Odinga mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya muungano huo, hadi pale Baraza Kuu, litakapoanza vikao vyake.

"Kabla ya Baraza Kuu kuanza rasmi vikao vyake, maamuzi yatakayofanywa na kiongozi wa Jubilee (Rais Kenyatta) na kiongozi wa ODM, Odinga yatachukuliwa kuwa maamuzi ya baraza," inasema katiba ambayo imepiga marufuku vyama wanachama kujiondoa miezi sita kabla ya uchaguzi mkuu na miezi mitatu baadaye.

Baraza Kuu pia lina jukumu ya kuongoza muungano wa Azimio na ndilo litatoa mwelekeo unaofaa kuchukuliwa na vyama wanachama.

Baraza pia limekubaliwa kusajili vyama vinavyohitaji kujiunga na muungano huo, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9, mwaka huu.

Chama cha Jubilee, kimeingia maelewano na zaidi ya vyama 10 ambavyo Rais Kenyatta atashughulikia maslahi yao, ndani ya muungano wa Azimio.

Ikimaanisha kuwa upande wa Rais Kenyatta huenda ukawa na wabunge wengi zaidi ikilinganishwa na vyama vingine ndani ya muungano, hivyo kuwa na usemi mkubwa.

Katibu Mkuu wa Jubilee Jeremiah Kioni, anasema chama hicho pia kitatoa mgombea mwenza wa Odinga katika juhudi za kutaka kuwa na usemi zaidi katika serikali ijayo.

Upande wa Naibu wa Rais, William Ruto, umekosoa hatua ya Rais Kenyatta kuteuliwa kuwa mwenyekiti wa hilo, huku ukidai kuwa hiyo ni ishara kwamba kiongozi wa nchi hana mpango wa kustaafu kutoka kwenye siasa baada ya kukamilisha muhula wake baada ya Uchaguzi Mkuu ujao.

Wazee wa jamii ya Wakikuyu mwezi uliopita walimuongezea Rais Kenyatta miaka mitano zaidi ya kuongoza jamii hiyo.

Chama cha Jubilee pia kilimteua Rais Kenyatta kuendelea kuwa kiongozi wake hata baada ya kustaafu.

### VIKWAZO VYAMKABILI ODINGA

Mvutano ndani ya muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya huenda ukavuruga ndoto ya mgombeaji wa urais Raila Odinga za kushinda katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Huku ikisalia miezi minne kabla ya Wakenya kuelekea upigaji kura. Odinga, anakabiliwa na kibarua cha kushughulikia matakwa mengi kutoka chama cha Wiper na vyama vingine vidogo katika muungano huo.

Hata baada ya muungano huo kusajiliwa rasmi katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa mapema wiki hii, chama cha Wiper bado kinapinga mambo kadhaa yaliyomo kwenye mkataba uliobuni muungano na muundo wa baraza kuu la uongozi.

Kwa mfano, chama hicho kinachoongozwa na makamu wa rais wa zamani, Kalonzo Musyoka kinapinga sehemu ya mkataba huo usemao vyama tanzu haviwezi kujiondoa kutoka Azimio miezi sita baada ya kusajiliwa kwake.

Pili, Musyoka anapinga hatua ya Odinga kuongeza idadi ya wanachama wa baraza kuu la muungano huo kutoka watu saba hadi 12, ili kujumuisha wawakilishi kutoka vyama vingine.

Musyoka amekuwa akiendeleza dhana kuwa Azimio ni muungano wenye mirengo mitatu mikuu; ODM, Jubilee na washirika wake na uliokuwa muungano wa One Kenya Alliance (OKA).

Kundi la viongozi wa vyama vingine wakiongozwa na Gavana Alfred Mutua (Machakos) na Kivutha Kibwana (Makueni) walilalamikia kile walichodai ni kutengwa katika kitovu cha kufanya maamuzi katika Azimio huku wakitishia kujiondoa.

Odinga alilazimika kufanya mazungumzo na kundi hilo ambalo lilibuni muungano mdogo kwa jina Mwanzo Mpya, likidai ndiyo nguzo ya nne katika muungano wa Azimio.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mitandao.***

# SHIME ATOA SIRI USHINDI SERENGETI GIRLS BURUNDI

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake chini ya miaka 17, (Serengeti Girls), Bakari Shime amesema vijana wake wamefanya kazi kwa juhudi na kufuata maelekezo jambo ambalo limewapa matokeo mazuri dhidi ya Burundi.

Serengeti Girls juzi iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya wenyeji wao Burundi, kwenye mchezo wa kwanza wa kufuzu Kombe la Dunia, mabao yakifungwa na Clara Luvanda aliyetupia mawili, Neema Paul na Husna Ayoub wakifunga moja kila mmoja.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema anafurahi kuona vijana wake wamefanya kazi nzuri katika mchezo huo na kupata ushindi ugenini.**

Alisema walijiandaa kwenda kukutana na mchezo mgumu hali ambayo imewasaidia kutoa ushindani mkubwa na kupata matokeo hayo yote yakichangiwa pia na kujituma na kujitolea kwa wachezaji wake.

"Mechi ilikuwa ya ushindani, niwapongeze vijana kwa kufanya kazi nzuri na kurudi nyumbani na ushindi na sasa tunarejea nyumbani kujipanga kwa mchezo wa marudiano," alisema kocha huyo.

Kwa matokeo hayo, Tanzania imejiwekea nafasi nzuri ya kufuzu Kombe la Dunia linalotarajiwa kufanyika nchini India baadaye mwaka huu.

Tanzania sasa imebakiza michezo mitatu ambayo ni pamoja na ule wa marudiano dhidi ya Burundi na kama itapata matokeo ya jumla itavaana na mshindi kati ya Zambia na Cameroon kwenye mechi za mwisho.





Mchezaji wa Chinoa FC (jezi ya njano) akiwania mpira dhidi ya mpinzani wake wa timu ya Raha Leo FC, kwenye mechi ya Ligi ya Mchangani ya Betika Sodo Bingwa, katika Kituo cha Mkoa wa Lindi, Ligi hiyo inayochezwa kwenye mikoa sita nchini imeingia mzunguko wa pili kwa udhamini wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Betika. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Care Boys yazidi kutisha Ligi ya Betika Sodo

Na Saada Akida

TIMU ya Care Boys imeendelea kuongoza msimamo wa Ligi ya Soka ya Mchangani 'Betika Sodo Bingwa', baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya 'ndugu' zao wa Kinondoni, Hard Number.

Mabao ya Care Boys katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Msisiri wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, yalifungwa na Shomari Kondo na Evalisto Noah.

Katika mchezo huo uliokuwa mkali na ushindani mkubwa, Hard Number walitangulia kupata bao la kuongoza katika dakika ya 30, kupitia kwa Awadhi Sudy, lakini katika kipindi cha pili Care Boys waligeuza matokeo kuwa 1-1 baada ya kusawazisha na kisha kufunga la ushindi.

Kocha wa Care Boys, Jaha Msome, akizungumzia matokeo mazuri ambayo wamekuwa wakiyapata, alisema kasi aliyoanza nayo wanahitaji kumaliza nayo ligi hiyo kabla ya kutangazwa ubingwa.

Alisema presha kubwa kwao wanaipata kutoka kwa Espanyola ambayo imekuwa na mwenendo mzuri katika ligi hiyo ya Betika Sodo Bingwa.

Mbali na mchezo huo pia kulitarajiwa kupigwa mechi nyingine, lakini Swaz Inter hawakutokea uwanjani hivyo kuwafanya wapinzani wao, Jaga FC kupewa alama tatu za bila kuzivujia jasho baada ya waamuzi kutekeleza kanuni za mashindano hayo.

Akizungumza kuhusu ligi hiyo kwa ujumla, Meneja Masoko wa Betika, Nelson Mwanuzi, alisema hamasa imekuwa kubwa kwa vijana kuchuana na kuonyesha vipaji vyao vya soka kwenye michuano hiyo inachezwa bila siku katika viwanja vya mchangani.

"Lengo kubwa ni kuibua vipaji kwa vijana katika mchezo huo wa soka la mchangani, lakini pia kuondoka wingi wa vijana mtaani kwa kupata kitu cha kufanya na kujiingizia kipato," alisema Mwanuzi.

Alisema Betika imeenda mbali kwa kuandaa ligi hiyo katika kila mkoa na kwamba wakati ikichezwa Dar es Salaam, pia inaendelea mikoani.

# Namungo FC, Ruvu Shooting zahofiana

Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango

LIGI Kuu Tanzania Bara raundi ya 20, itaendelea leo kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi, kati ya wenyeji Namungo FC dhidi ya Ruvu Shooting, ambazo kila moja imeonesha hofu ya kupata alama tatu.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Klabu ya Namungo, Jamhuri Kihwelu 'Julio', amesema mchezo huo utakuwa mgumu, lakini wamejipanga kukabiliana na kila aina ya ushindani ili kupata alama tatu.

Akizungumzia mchezo huo jana, Julio alimwambia mwandishi wetu kuwa ugumu huo unaongezwa na uhalisia kwamba, kwa sasa hakuna timu yoyote ya kubeza kutokana na ligi hiyo kuelekea ukiongoni.

"Mchezo utakuwa mgumu kutokana na aina ya timu tunazokutana nazo lakini tumejipanga kupata pointi tatu," alisema Julio na kuongeza kuwa makosa machache yaliyojitokeza kwenye mechi zilizopita tayari wameyafanyia kazi.

Wakati Julio akiyasema hayo, Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Mbwire, pia alionekana naye kuwahofia Namungo, akidai kuwa itakuwa ni mechi ngumu kwani wenyeji wao ni timu nzuri.

Masau alisema wanakwenda kucheza na timu bora ya Namungo, ambayo licha ya kuwa hivyo, lakini ina wachezaji wazuri na wenye uwezo wa hali ya juu wa kitaifa na kimataifa, hivyo inabidi waingie kwa tahadhari kubwa kwa kama lengo lao ni kusogea kwenye nafasi za juu.

"Utakuwa mchezo mgumu sana kwa sababu Namungo wako vizuri hata kwenye msimamo wa ligi, kwa hiyo watataka kushinda mechi hiyo ili wapae juu kwa kuwa wanataka kupata nafasi tatu au nne za juu. Pamoja na hayo na sisi pia tunataka kushinda mechi hiyo ili kutoka hapa tulipo na kusogea juu, lengo letu ni kwamba ligi ikimalizika tuwe sehemu salama kimsimamo," alisema msemaji huyo.

Namungo iko kwenye nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imecheza mechi 19, ikikusanya pointi 26, huku Ruvu Shooting ikiwa nafasi ya 11 kwa pointi 21 ilizonazo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU RUKSA KUONDOKA

CHELSEA wanajiandaa kumuacha Mshambuliaji wao Mbelgiji, Romelu Lukaku aondoke katika klabu hiyo msimu huu, huku Inter Milan na Paris St-Germain zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(90 Min)***

### ZIDANE KOCHA MPYA PSG

KLABU ya Paris Saint-Germain, tayari imeshindwa kuelewana na Mauricio Pochettino na wanamatumaini ya kumteua Zinedine Zidane kama kocha wao mpya. ***(Le Parisien)***

### BARCA WAMRUDIA MARTINEZ

BARCELONA wamerejea katika kinyang'anyiro cha kutaka kumsajili, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24 kutoka Inter Milan. ***(Sport)***

### BEI YA HENDERSON YATAJWA

MANCHESTER United wameweka bei ya pauni milioni 40 kwa golikipa wao, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 25, ambaye yuko tayari kuondoka Old ttraford msimu huu, huku Newcastle ikiwa ni miongoni mwa klabu zinazomlenga. ***(Star)***

### HAG NA VAN PARSIE

KOCHA ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag atamchukua msaidizi wake wa Ajax, Mitchell van der Gaag kwenda naye pale Old Trafford, lakini Robin van Persie bado hajaamua juu ya ofa ya kumtaka ajiunge naye katika klabu hiyo. ***(Mirror)***

### DIOP AWANIWA LYON

MLINZI wa West Ham, Issa Diop mwenye umri wa miaka 25, amejitokeza kama mchezaji anayelengwa na Lyon kuhamia katika klabu hiyo. ***(L'Equipe)***

### CITY WAKOMAA NA HAALAND

MANCHESTER City wamefanya mazungumzo zaidi juu ya pendekezo la kumsajili, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia. ***(Star)***

### MADRID WAMECHELEWA

REAL Madrid wamechelewa katika uamuzi wao wa kutaka kumsajili, Erling Haaland ambaye anawania na klabu za Ligi Kuu England. ***(Sport)***

### ROMA KUAMUA KWA ZANIOLO

AS Roma wanaangalia uwezekano wa kumuachia kiungo wa kati, Nicolo Zaniolo aondoke mwishoni mwa msimu na wataangalia uwezekano wa ofa watakayopewa na klabu za Serie A na Ligi Kuu England zinazomtaka mchezaji huyo. ***(Corriere dello Sport)***

### RAMSAY AMULIKWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanamuwania nyota wa klabu ya Aberdeen Mskochi, Calvin Ramsay na wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, kuziba nafasi ya Trent Alexander-Arnold. ***(Sun)***

### JANELT AANIKA ANAKOTAKIWA

KIUNGO wa kati wa Brentford, Vitaly Janelt mwenye umri wa miaka 23, amesema amekuwa na mawasiliano kutoka klabu za Ligi Kuu England na Ujerumani. ***(Kicker)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZE... ULAYA



# ARTETA AKATA TAMAA ARSENAL KUFUZU UEFA

**Inakatisha tamaa sana, na ni vigumu kueleza kwa maneno, lakini huu ni mchezo wa soka...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alielezea kichapo cha Arsenal cha bao 1-0 kwenye Ligi Kuu England kutoka kwa Southampton kama fursa "kubwa" iliyokosa kwenye harakati zao za kutafuta nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Jan Bednarek alifunga bao pekee katika mchezo huo na kuwafanya 'Washikabunduki' hao kupoteza mchezo wao watatu mfululizo wa Ligi Kuu.**

Arsenal wangefikisha pointi sawa na Tottenham Hotspur waliopo nafasi ya nne kama wangeshinda, huku kikosi cha kocha Antonio Conte kikipoteza kwa dakika za mwisho mbele ya Brighton na Hove Albion mapema siku hiyo.

Kwa hali ilivyo, walimaliza wakiwa nafasi ya sita baada ya ushindi wa mabao 3-2 wa Manchester United dhidi ya Norwich City na kuwafanya vijana wa Ralf Rangnick kuwaruka Arsenal hadi nafasi ya tano.

Arsenal ndio ilikuwa timu iliyotawala zaidi pale St Mary's, wakipiga mashuti 23 na kumiliki mpira kwa asilimia 76. Ingawa amechanganyikiwa kwa kukosa nafasi ya kuchukua fursa ya kuteleza kwa Tottenham, Arteta anaamini siku nyingine timu yake itapambana kushinda.

Alipoulizwa kama ilikuwa ni nafasi aliyokosa, Arteta alijibu: "Sawa, kwa sababu kwa mtu ambaye hajui matokeo na anatazama mchezo, unajua watakuambia nini ... kwamba Arsenal walishindwa mchezo. Haikufanya hivyo. Inakatisha tamaa sana, na ni vigumu kueleza kwa maneno.

"Lakini huu ni mchezo wa soka unaoufanya kuwa tofauti na mwingine wowote, kwa sababu kwenye mpira wa kikapu ni tofauti.

"Walifunga bao moja, na kwa muda ambao tulitumia kuzunguka eneo la hatari, mashuti tuliyopata, hali na nafasi za wazi ambazo tulipata, unashindwa kuelewa.

"Lazima tushinde mechi za soka na tufunge mabao zaidi, na hilo ni tatizo tulilonalo kwa sasa."

Arsenal ilianza na wachezaji watatu wa mbele Eddie Nketiah, Gabriel Martinelli na Bukayo Saka, huku Alexandre Lacazette akijitenga baada ya kukutwa na COVID-19.

Arteta alikataa kuwakosoa watatu hao, lakini akapendekeza Arsenal haingeambulia patupu kama mshambuliaji mwenye uzoefu zaidi angekuwa uwanjani.

"Ni kile tulichonachọ," aliongeza. "Wachezaji tulionao hawajafanya hivyo kwenye ligi hii, unapokuwa na mchezaji wa kiwango cha kimataifa ambaye anacheza ligi kwa miaka 10, unakuwa na uhakika wa kupata chochote."

Arsenal watarejea katika mechi ya Ligi Kuu Jumatano watakaposafiri hadi Stamford Bridge kwa mchezo dhidi ya Chelsea, kabla ya kumenyana na Manchester United nyumbani Jumamosi ijayo.

SportPesa LIVE IN PLAY

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
CADIZ CF
1 | 1.26
X | 5.65
2 | 10.93

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GUARDIOLA AOTA USHINDI LIVER KWA MAN CITY

**LONDON,** England

MANCHESTER City walijitoa kwa kila kitu wakati wakifungwa na Liverpool kwenye nusu fainali ya Kombe la FA Jumamosi, kwa mujibu wa Pep Guardiola.

City walichapwa mabao 3-2 katika mchezo huo uliopigwa Uwanja Wembley huku timu ya Jurgen Klopp ikichukua nafasi ya kujivunia katika pambano hilo na kutinga fainali ya 15 ya Kombe la FA, ingawa ya kwanza tangu mwaka 2012 (Manchester United na Arsenal ndio timu pekee zilizocheza fainali nyingi zaidi ya mashindano hayo).


Siku sita baada ya sare ya kusisimua ya mabao 2-2 kati ya City na Liverpool kwenye Ligi Kuu, timu iliyobadilika sana kutoka kwa Guardiola ilijikuta ikifungwa 3-0 hadi mapumziko.

Ibrahima Konate aliiweka Liverpool mbele mapema na Sadio Mane akaongeza la pili wakati golikipa namba mbili wa City, Zack Steffen alipofanya makosa.

Jack Grealish aliirudisha City mchezoni kabla ya Bernardo Silva kufunga la pili, lakini bahati haikuwa upande wao.

"Kazi yetu ilikuwa katika kipindi cha pili," alisema Guardiola akiiambia BBC Sport mara baada ya mchezo huo.

"Tulikuwa na nafasi za kusawazisha. Ilikuwa mechi ngumu kwa sababu tumetoka kwenye michezo tuliyocheza siku tano au sita zilizopita. Vijana walijiweka sawa.




## 'Utd haitakiwi kumtegemea CR7'

**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick amesema Manchester United haiwezi kumudu kumtegemea Cristiano Ronaldo pekee licha ya hat-trick yake ya ushindi wa mechi dhidi ya Norwich City.

Ronaldo alifunga hat-trick ya 50 katika maisha yake ya soka na kuiongoza United kwa mabao 2-0 kabla ya kuhitimisha ushindi huo kwa mkwaju wa faulo.

Mshambulizi huyo amefunga mabao 15 katika mechi 26 za Ligi Kuu msimu huu, akichangia asilimia 28.8 ya mabao ya 'Mashetani Wekundu' hao.

Licha ya mabao matatu ya Ronaldo kuisogeza United hadi ndani ya pointi tatu dhidi ya Tottenham walio katika nafasi ya nne baada ya wao na wapinzani wao wa London Kaskazini, Arsenal kupokea kichapo cha kushitukiza, Rangnick alisikitishwa na kuendelea kwa timu yake kumtegemea mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37.

Kocha huyo wa muda pia alionesha kukerwa kwake na safu ya ulinzi ya United baada ya mabao ya Keiran Dowell na Teemu Pukki kutishia mabadiliko ya kushangaza pale Old Trafford.

"Ilikuwa mara ya pili sasa (ambapo Ronaldo alifunga bao la tatu la ushindi) kama dhidi ya Spurs na matokeo sawa, 3-2 kama leo," alisema Rangnick akiiambia BBC Sport.

"Lakini hatupaswi kumtegemea yeye tu.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# YANGA PRINCESS YAANZA KULIA PENGO LA MASAKA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 3-2 na Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Kocha wa Muda wa Yanga Princess, Fred Mbuna, amesema moja ya sababu ya kupoteza ni kuondokewa na straika wao hatari, Aisha Masaka aliyekwenda kucheza soka la kulipwa nchini Sweden.

Kauli hiyo ya Mbuna ambaye alikaimu nafasi hiyo kwa muda kutokana na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Edna Lema, kuwa na majukumu na kikosi cha timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), inakinzana na Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Khalifan Mbonde.

Katika mchezo uliopita ambao Yanga Princess iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Alliance Girls kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Mbonde alisema kuondoka kwa Masaka hakujaacha pendo ndani ya kikosi chao kwa kuwa washambuliaji waliopo wameweza kuliziba vema.

**Lakini pia wakati Yanga Princess ikikutana na kipigo hicho mwishoni mwa wiki huku Mbuna akisema kimetokana na kutokuwapo kwa Masaka, siku moja kabla watani zao wa jadi, Simba Queens, walitoa kipigo cha mabao 7-0 dhidi ya Oysterbay Queens bila kuwapo kwa straika wao, Opah Clement ambaye naye yupo nchini Uturuki akifanya majaribio ya kucheza soka la kulipwa.**

“Tumefanya makosa tumeadhibiwa, lakini hii ni mechi ya pili ya raundi ya pili, tutaendelea kurekebisha makosa ili tuweze kufanya vizuri, bado akili yetu ipo kwenye ubingwa kwa sababu hata timu inayoongoza inaweza kuteleza pia,” alisema Mbuna, beki wa zamani wa Yanga na Majimaji huku akikiri.

“Pengo la Masaka linaonekana wazi kabisa, na pia tuna mchezaji wetu mwingine yupo kwenye timu ya taifa ya wanawake, lakini sisi tunaendelea na ligi na huwezi kusema tusicheze, kwa hiyo kukosena kwao athari ipo. Haiwezekani mchezaji wa kutegemewa, mwingine anachaguliwa mpaka kwenye timu ya taifa, asilete athari kwenye timu kama akikosena,” alisema.

Pamoja na kipigo hicho, Yanga Princess inasalia kwenye nafasi ya tatu kwa pointi zake 29, Fountain Gate ikiwa ya pili kwa pointi 34, Simba Queens ikiendelea kuteza kileleni kutokana na kukusanya pointi 39.




Nahodha wa timu ya Simiyu Veterans, Marko Matogoro (kushoto), akipokea kombe kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, baada ya kuibuka mabingwa kwenye mechi ya fainali ya Kilele cha Bonanza la Pasaka 2022 dhidi ya Kahama Veterans iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi. Simiyu Veterans ilishinda kwa mabao 3-1. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Simiyu Veterans mabingwa Pasaka

**Na Happy Severine,** BARIADI

TIMU ya soka ya Simiyu Veterans, imetwaa ubingwa wa michuano ya Bonanza la Pasaka, lililoshirikisha timu kumi kutoka mikoa 10 ya Kanda ya Ziwa na kufanyika mkoani Simiyu.

Simiyu Veterans, ilitwaa ubingwa huo baada ya kuwacharaza mabao 3-1 timu ya Kahama Veterans katika mechi ya fainali ya kilele cha bonanza hilo, iliyopigwa kwenye Uwanja wa Halmashauri Mji wa Bariadi juzi.

Akikabidhi kombe hilo kwa washindi hao, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi Lupakisyo Kapange kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alisema ushindi huo umewapa heshima kubwa na kuahidi kusaidia maandalizi ya bonanza hilo kila mwaka.

Kapange alisema kwa kutambua kuwa michezo ni afya, watahakikisha wanaboresha miundombinu ya michezo hiyo ili iwe wezeshi kwa kujenga viwanja bora na vya kisasa.

Pia alizitaka kila halmashauri kuhakikisha inatenga na kujenga viwanja vya mipira ili kukuza zaidi vipaji vya vijana ambao watashiriki mashindano ya kitaifa.

Katibu wa Simiyu Veterans, Ibrahim Kadudu, ambao ni waandaaji wa michuano hiyo, alisema lengo la bonanza hilo ni kujenga uhusiano na timu zingine huku akitoa kilio cha uhaba wa waamuzi na viwanja vya kuchezea kuwa ni changamoto na kumuomba mgeni rasmi kuwasaidia kutatua hayo kwa haraka.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 18/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2676 | Middlesbrough vs Huddersfield | 1.79 | 3.45 | 4.34 |
| 15:00 | 4417 | Vejle BK vs Nordsjalland | 2.31 | 3.44 | 2.84 |
| 15:00 | 4667 | Sonderjyske vs Aarhus | 2.84 | 3.39 | 2.34 |
| 15:15 | 4304 | FC Luzern vs St. Gallen | 2.53 | 3.42 | 2.58 |
| 16:00 | 1857 | Slask Wroclaw vs Wisla Krakow | 2.22 | 3.20 | 2.96 |
| 16:00 | 5950 | KAA Gent vs Anderlecht | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 17:00 | 1065 | Millwall vs Hull City | 1.82 | 3.33 | 4.37 |
| 17:00 | 1243 | Reading vs Swansea | 2.56 | 3.25 | 2.61 |
| 17:00 | 1345 | Coventry vs Bournemouth | 3.03 | 3.23 | 2.27 |
| 17:00 | 1884 | Cardiff vs Luton Town | 2.77 | 3.17 | 2.48 |
| 17:00 | 2681 | Blackpool vs Birmingham | 2.12 | 3.22 | 3.37 |
| 17:00 | 3371 | Blackburn vs Stoke City | 1.91 | 3.32 | 3.91 |
| 17:00 | 3904 | QPR vs Derby | 2.17 | 3.23 | 3.23 |
| 17:00 | 4548 | Barnsley vs Peterborough | 1.95 | 3.32 | 3.76 |
| 17:30 | 3617 | FC Sion vs FC Basel | 3.48 | 3.68 | 1.94 |
| 17:30 | 3896 | Lausanne-Sport vs FC Lugano | 2.89 | 3.24 | 2.37 |
| 18:00 | 1342 | VPS Vaasa vs HJK Helsinki | 6.43 | 3.99 | 1.44 |
| 18:00 | 3010 | Hifk vs Lahti | 2.20 | 3.26 | 2.96 |
| 18:00 | 3923 | Dalkurd FF vs Halmstads BK | 3.47 | 3.37 | 2.10 |
| 18:00 | 4225 | Orgryte IS vs Osters IF | 2.38 | 3.23 | 3.03 |
| 18:00 | 4893 | IFK Mariehamn vs Honka | 3.07 | 3.12 | 2.20 |
| 18:00 | 5444 | PAS Giannina vs AEK Athens | 4.98 | 3.33 | 1.74 |
| 18:30 | 2487 | Gornik Zabrze vs Lechia Gdansk | 2.06 | 3.16 | 3.35 |
| 19:00 | 1006 | Parma vs Ascoli | 2.05 | 3.26 | 3.51 |
| 19:00 | 1444 | Pisa vs Como | 1.61 | 3.66 | 5.35 |
| 19:00 | 1907 | Cittadella vs Alessandria | 2.04 | 3.22 | 3.57 |
| 19:00 | 3053 | Odd Ballklubb vs Viking | 2.53 | 3.42 | 2.58 |
| 19:00 | 3130 | Ternana vs Frosinone | 2.68 | 3.22 | 2.53 |
| 19:00 | 3476 | Haugesund vs Stromsgodset | 2.14 | 3.44 | 3.14 |
| 19:00 | 4656 | Ham-Kam vs Sandefjord | 2.32 | 3.34 | 2.89 |
| 19:00 | 4896 | Aalesunds vs Tromso | 2.28 | 3.33 | 2.98 |
| 19:00 | 5104 | Jerv vs Kristiansund | 2.95 | 3.35 | 2.29 |
| 19:00 | 5121 | Midtjylland vs Aalborg | 1.85 | 3.54 | 3.99 |
| 19:00 | 5176 | Sarpsborg vs Rosenborg | 2.49 | 3.33 | 2.68 |
| 19:00 | 5371 | Molde vs Lillestrom | 1.54 | 4.28 | 5.18 |
| 19:30 | 5325 | Bristol City vs Sheffield Utd | 3.97 | 3.68 | 1.80 |
| 20:00 | 1068 | Napoli vs Roma | 1.88 | 3.56 | 3.91 |
| 20:00 | 1375 | Girona vs Real Sociedad B | 1.57 | 3.80 | 5.53 |
| 20:30 | 3984 | Galatasaray vs Yeni Malatyaspor | 1.29 | 5.18 | 9.16 |
| 21:00 | 2033 | Legia Warszawa vs GKS Piast Gliwice | 2.41 | 2.97 | 2.87 |
| 21:00 | 4078 | Shamrock Rovers vs Dundalk FC | 1.53 | 3.90 | 5.26 |
| 21:00 | 4813 | Bodo Glimt vs Valerenga | 1.45 | 4.57 | 5.97 |
| 21:30 | 3586 | Monza vs Brescia | 2.15 | 3.22 | 3.27 |
| 22:00 | 1974 | Nottingham vs West Bromwich | 1.98 | 3.31 | 3.65 |
| 22:00 | 3035 | Atalanta vs Verona | 1.61 | 4.08 | 4.88 |
| 22:00 | 3835 | Barcelona vs Cadiz CF | 1.26 | 5.65 | 10.93 |
| 22:30 | 2806 | Misr Lel Makasa vs Ghazl EL Mahallah | 3.58 | 2.93 | 2.20 |
| 22:30 | 3545 | Farco FC vs Arab Contractors | 2.04 | 2.99 | 3.99 |
| 22:30 | 5777 | GD Estoril vs Sporting Braga | 3.62 | 3.33 | 2.01 |
| 23:00 | 2997 | Leones FC vs Orsomarso | 1.45 | 4.07 | 6.01 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Aprili 18, 2022

Nipashe




Arteta akata tamaa kufuzu Uefa UKURASA 21

IMEISHA HIYO...




Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao pekee kwa mkwaju wa penalti wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Penalti hiyo ilitokana na Bernard Morrison kuchezewa madhambi ndani ya 18. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Nabi aiacha Simba, akili kwa Namungo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kwa sasa hafikirii kabisa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Simba kwani akili yake sasa ameigeuzia kwanza kusaka pointi tatu dhidi ya Namungo FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mechi ya 'Kariakoo Derby', anaichukulia kwa hisia kubwa na muhimu, lakini wanahitaji kuelekeza nguvu zaidi katika mchezo ujao dhidi ya Namungo FC.

Alisema wanahitaji kufikiria zaidi mechi hiyo iliyopo mbele yao watakayocheza Jumamosi wiki hii dhidi ya Namungo kwani ni muhimu kutafuta pointi tatu kwa sababu iliwasumbua katika mzunguko wa kwanza.

"Kwa misimu yote Namungo imekuwa ikitusumbua iwe tunacheza nyumbani au ugenini, lazima tuelekeze nguvu na akili zetu katika mchezo huo kabla ya kuwafikiria Simba kwa sasa.

"Wachezaji wanatambua kwamba sasa tunatakiwa kuangalia kilichopo mbele yetu ikiwa ni mchezo wetu dhidi ya Namungo FC kwanza, ili kuhakikisha tunaendelea kupata matokeo mazuri baada ya hapo ndiyo tutafikiria Derby," alisema Nabi.

# Simba yanusa nusu fainali CAF

## Morrison, Kapombe wainusisha Orlando 'pumzi ya moto' kwa Mkapa, sasa wahitaji sare tu...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la mkwaju wa penalti iliyowekwa nyavuni dakika ya 67 na beki wa kulia, Shomari Kapombe jana usiku, liliwapa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ushindi wa 1-0 dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini na hivyo kutanguliza mguu mmoja nusu fainali ya michuano hiyo.

**Ilikuwa ni mechi ya kwanza ya robo fainali Kombe la Shirikisho, huku marudiano yakitarajiwa kuchezwa Jumapili wiki hii nchini Afrika Kusini na mshindi wa jumla atatinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani Afrika.**

Japo ni ushindi kiduchu, lakini uliendeleza rekodi nzuri ya Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakiendeleza kaulimbiu yao ya 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu', ikiwa na maana kila anayekanyaga kwenye uwanja huo, hatoki salama katika michuano ya kimataifa.

Penalti hiyo ilipatikana dakika ya 64, baada ya winga mtukutu, Bernard Morrison kuangushwa ndani ya aneo la hatari na mwamuzi kuamuru mkwaju wa penalti, Kapombe akimhadaa kipa Richard Ofori, aliyeruka kulia na mpira ukatinga kushoto kwake.

Dakika ya kwanza tu, Kapombe huyo huyo alitaka kumjaribu kipa Ofori kwa kupiga shuti la mbali, lakini lilitoka nje ya lango.

Dakika saba baadaye kosa lililofanywa na Mohamed Hussein kuukosa mpira, lilimfanya Siphesile Ndlolu kuunasa na kuambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto kuelekea langoni mwa Simba, lakini alikuwa mchoyo akataka kupiga mwenyewe, shuti lake likatoka nje.

Orlando Pirates ilicheza mfumo wa kujikusanya nyuma, wakizuia zaidi, lakini walipokuwa wakiupata mpira walisambaa na walipokuwa wakiupoteza, wakirejea wote nyuma kuzuia, kitu ambacho kiliwafanya wachezaji wa Simba kuwa na mpira muda mwingi wa mchezo kipindi cha kwanza, lakini walishindwa kupata mbinu mbadala ya kuipenya ngome ya wapinzani wao hao.

Kwame Pepara, raia wa Ghana alirushiwa mpira akiwa karibu na lango la Simba dakika ya 33, akageuka ghafla na kuwahadaa mabeki, kabla ya kupiga shuti dhaifu, lakini la hatari, lililodakwa vema na kipa Aishi Manula.

Mashambulizi machache ya kushtukiza ya Orlando Pirates yalizidi kuleta hatari kwenye lango la Simba, kwani dakika tatu kabla ya mechi kwenda mapumziko, kulitokea kizaazaa lango la wenyeji kiasi cha kusababisha Kapombe na Ndlovu kuumia, lakini walirejea uwanjani.

Shambulizi la hatari zaidi ambalo Simba ililifanya kipindi chote cha kwanza lilikuwa ni dakika moja kabla ya mechi kwenda mapumziko baada ya Morrison kuupata mpira karibu na eneo la hatari, akageuka na kuvuta hatua chache, kabla ya kuachia shuti kali, shukrani kwa kipa Ofori ambaye aliruka na kuupangua, ikawa kona ambayo haikuwa na manufaa yoyote.

Kipindi cha pili, wageni walionekana kufunguka na kuanza kulishambulia lango la wenyeji wao, lakini mabeki Henock Inonga na Paschal Wawa ambaye alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu jana, walikaa imara kuzima mashambulizi ya Deon Hotto, Kabelo Dlamini, Kwame na Thabang Monare.

Kufunguka kwao, ndiko kulisababisha kuruhusu kushambuliwa na hata baada ya hapo, walionekana kutaka kupata bao la kusawazisha.

Ilibidi wa Kocha wa Simba, Pablo Franco afanye mabadiliko kwa kuwatoa Peter Banda, Thadeo Lwanga, Pape Sakho, Chris Mugalu na Morrison ambaye aliumia na nafasi zao zikachukuliwa na Kibu Denis, Rally Bwalya, Meddie Kagere, Yusuph Mhilu na Mzamiru Yassin ambao kwa kiasi kikubwa walisaidia kutuliza presha ya mechi na dakika 90 zikamalizika kwa ushindi wa bao hilo.

Ili Simba itinge nusu fainali, inapaswa itoke sare yoyote ama ishinde kwenye mechi ya marudiano nchini Afrika Kusini Jumapili wiki hii.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >